SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII, BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Naibu** Waziri aitaka Tanesco kujitathmini katika utendaji wake

UKURASA 4



**Diamond, Harmonize watunishiana misuli**

UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Januari 1, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580812
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_n
LIKE & F

# Hoja saba za Samia Mwaka Mpya



• **Dk.** Mwinyi asisitiza kuchapa kazi, mapambano dhidi ya corona, rushwa...

*Endelea ukurasa 3 & 5*

## Adaiwa kumuua mumewe kwa maji moto na petroli

UKURASA 4




## Matarajio mapya mwaka 2022

UKURASA 2

MICHEZO **SIMBA, AZAM FC HATUMWI MTOTO** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Matarajio ya Mwaka 2022



Humphrey Polepole



Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe,

**Na Sanula Athanas**

LEO ni siku ya kwanza ya Mwaka 2022, ikikumbusha kwamba imebaki miaka mitatu kabla ya kufika ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999 hadi mwaka 2025.

Dira hiyo pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Wakati mwaka mpya huo ukianza huku dunia ikikumbuka imebaki miaka minane kabla ya kuufikia ukomo wa kipindi cha Malengo ya Maendeleo Endelevu, Tanzania kunatarajiwa kuwa na mambo kadhaa mwaka huu yanayogusa nyanja za kisiasa, kiuchumi na kijamii.

**CHAGUO LA PILI SEKONDARI**

Miaka mitatu mfululizo iliyopita kulishuhudiwa aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Seleman Jafo, kila ilipofika Desemba akiwabana wakuu wa mikoa, wilaya na wakurugenzi watendaji wa halmashauri kusimamia ujenzi wa madarasa kwa ajili ya wanafunzi waliofaulu kujiunga na sekondari lakini hawakuchaguliwa kutokana na uhaba wa madarasa.

Mwaka huu serikali imeepuka fedheha hiyo, Waziri mpya, Ummy Mwalimu, akitangaza kuwa mwaka huu (2022) hakutakuwa na mwanafunzi wa kidato cha kwanza atakayelazimika kukaa nyumbani kusuburi madarasa kujengwa, fedha za tozo za miamala ya simu na mkopo wa kukabiliana na athari za UVIKO-19 zikielekezwa kwenye ujenzi huo wa madarasa na shule shikizi.

**TUME HURU UCHAGUZI**

Pande zote zilizokutana jijini Dodoma mwezi uliopita katika mkutano wa wadau wa demokrasia, zilikubaliana nchi iwe na tume huru ya kusimamia Uchaguzi Mkuu na kuimarisha demokrasia nchini.

Tayari kumeundwa jopo la kufanyia kazi hoja zilizowasilishwa na wadau washiriki zikigusa maeneo mengine nyeti ikiwamo kudai kuruhusiwa kwa mikutano ya hadhara ya kisiasa.

Utekelezaji wa hoja hizo zinazogusa moja kwa moja utengamano wa kisiasa nchini huenda ukashuhudiwa mwaka huu.

**LISSU KUREJEA**

Septemba 7, 2017 Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu alishambuliwa kwa risasi jijini Dodoma na kulazimika kupelekwa Nairobi, Kenya na baadaye Ubelgiji kwa ajili ya matibabu ya kibingwa.

Lissu amekuwa akiishi Ubelgiji hadi sasa japo Julai 27, 2020 alitua nchini na kushiriki kampeni na Uchaguzi Mkuu kisha kurejea Ubelgiji muda mfupi baada ya uchaguzi huo kutokana na kile alichodai hofu ya usalama wake.

Mtaalamu huyo wa sheria alikariri jana akibainisha kuwa ana mpango wa kurejea nchini mwaka huu na ataongeza nguvu kwenye jopo la mawakili wanaomtetea Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake katika kesi ya Uhujumu Uchumi.

**HATIMA KINA POLEPOLE**

Wabunge watatu ambao ni wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM): Humphrey Polepole (Kuteliuwa), Askofu Josephat Gwajima (Kawe) na Jerry Silaa (Ukonga) wanakabiliwa na tuhuma za kukiuka maadili ya chama hicho.

Tayari wabunge hao wamehojiwa na kamati kadhaa, ikiwamo Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, huku Kamati Kuu ya CCM ikipitia taarifa za kamati zilizowahoji na kuagiza waitwe kujitetea mbele yake. Hatima ya wabunge hao inatarajiwa kujulikana mwaka huu.

**NJAA, UKAME**

Athari za mabadiliko ya tabianchi zimeonekana dhahiri kwenye maeneo mengi nchini, kukishuhudiwa kuchelewa kwa mvua, joto kali na ukame kwenye maeneo mengi huku huduma za maji na umeme nazo zikisuasua katika baadhi ya maeneo.

Mwaka huu kunatarajiwa kuwa na hali ya ukame na njaa kwenye maeneo mengi, tahadhari hiyo ilishawekwa bayana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA).

**KASI YA MIRADI**

Kuyumba kwa uchumi wa nchi nyingi kuliibua hofu katika utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati nchini, lakini katika hotuba yake ya mwanzoni mwa wiki hii, Rais Samia Suluhu Hassan aliwahakikishia wananchi kuwa "hakuna mradi utakaoachwa" na kwamba serikali imeshatoa fedha na inachodai ni utekelezaji wa miradi kwa makandarasi.

**MAPAMBANO CORONA**

Tanzania iliripoti kupata mgonjwa wa kwanza wa virusi vya corona Machi 16, 2020 na madhara ya virusi hivyo yameonekana kwenye sekta karibu zote.

Kwa sasa serikali inaendelea kutekeleza afua mbalimbali kukabiliana na UVIKO-19, ikiwa ni pamoja na kuhimiza wananchi kupata chanjo dhidi ya ugonjwa huo. Mwaka huu kunatarajiwa kushuhudiwa mikakati zaidi ya kukabiliana na baa hilo.

**HATIMA MBOWE, SABAYA**

Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amekata rufani kupinga hukumu ya miaka 30 jela iliyotolewa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha mwaka jana huku akikabiliwa na kesi nyingine ya Uhujumu Uchumi kwenye mahakama hiyo.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Mbowe, anakabiliwa na kesi ya Uhujumu Uchumi katika Mahakama Kuu Divisheni ya Uhujumu Uchumi. Hatima ya wanasiasa hao wawili inatarajiwa kujulikana mwaka huu.

**MRITHI WA MAALIM SEIF**

Februari 17 mwaka jana, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Chama cha ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharrif Hamad, alifariki dunia.

Tayari nafasi yake ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar imeshajazwa lakini ACT-Wazalendo haijachagua mrithi wa kiti chake ndani ya chama. Chama hicho kinatarajiwa kukamilisha mchakato huo mwaka huu.

**MABADILIKO UONGOZI**

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anaendelea kutumbua viongozi na kuteua wapya na katika mkutano wake na wahariri mwezi uliopita Ikulu Zanzibar, aliweka wazi kuwa mabadiliko kwenye Baraza la Mawaziri na uongozi wa mashirika na taasisi za umma hayaepukiki.

Mwaka huu kunatarajiwa kuwa na mabadiliko kwenye nafasi hizo huku wanawake wakitarajiwa kupewa nafasi zaidi katika utekelezaji wa mkakati wa kuwa na usawa kijinsia. Mabadiliko hayo pia yanatarajiwa kuonekana kwenye uchaguzi wa viongozi wa CCM.

**WABUNGE 19 CHADEMA**

Hatima ya wabunge 19 wanaotokana na CHADEMA pia inatarajiwa kujulikana mwaka huu. Wabunge hao wameshakata rufani kwenye vikao vya juu vya chama hicho lakini vikao hivyo havijaitishwa kushughulikia suala lao.

Spika Job Ndugai alisisitiza mara kadhaa mwaka jana kwamba taratibu za kuwavua ubunge huo hazijafuatwa na chama chao kutokana na dosari alizobaini kwenye barua zilizotumwa kwake na Ofisi ya Katibu Mkuu wa chama hicho.

HABARI KITAIFA

# Hoja saba za Samia Mwaka Mpya 2022

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan amelihutubia taifa usiku wa kuamkia leo, akisisitiza mambo saba muhimu kwa wananchi wanapouanza mwaka mpya wa 2022.

Katika hoja yake ya kwanza, Rais Samia alisema serikali ina utazama mwaka 2022 kuwa ni mwaka wa kukabiliana na kero zinazopunguza uwezo wa wananchi katika kukabiliana na maisha ya kila siku.

"Kama ilivyotamkwa kwenye Mpango wa Tatu wa Serikali wa Miaka Mitano wa 2021/2026, kwamba lengo kuu ni kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na uchumi wa taifa kwa ujumla," alisema.

Rais alisema dunia bado inakabiliwa na UVIKO - 19 na kwa sasa iko katika wimbi la nne la ugonjwa huo, akibainisha kuwa kirusi kipya cha Omicron kinaenea kwa kasi kubwa na tayari kipo na kimeshaingia nchini.

"Niwakumbushe kuchukua tahadhari kwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya. Pia, nitumie fursa hii kuwahimiza wananchi kupata chanjo dhidi ya UVIKO - 19," alisema.

Katika hoja yake ya tatu, Rais Samia alikumbusha kuwa mwaka huu ni wa Sensa ya Watu na Makazi, hivyo kuwahimiza Watanzania kujitokeza kuhesabiwa ili kupata takwimu zitakazosaidia katika kupanga kwa usahihi masuala ya maendeleo.

Alilitaja jambo la nne la kutiliwa mkazo mwaka huu ni watumishi wote wa umma na sekta binafsi kuuanza mwaka mpya wakiwa na lengo la kuongeza ufanisi katika uzalishaji na ubora katika utoaji wa huduma.

"Kwa wazazi wenzangu, nawasihi msijisahau na tafrija na sherehe za sikukuu ni vyema mkatumia muda huu kuwaandaa watoto wetu kukabiliana na changamoto mpya za kimasomo, na kuhakikisha kwamba hawaikosi fursa adhimu ya elimu bila malipo inayotolewa na serikali yao," alisema Rais Samia katika hoja yake ya tano.

Mkuu wa Nchi pia alitoa angalizo kwa wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ajali za barabarani wakati wa kurejea maeneo yao ya kazi kutoka mapumziko ya sikukuu za mwishoni mwa mwaka, ili kupunguza ajali zinazoepukika ambazo mara nyingi humaliza nguvu kazi ya taifa.

Katika hoja yake ya saba, Rais Samia alihimiza uadilifu katika kulitumikia taifa, huku akiwatakia Watanzania wote heri, fanaka na mafanikio katika Mwaka Mpya wa 2022 na kuwataka wamwombe Mungu ili ashushe neema na baraka na kuwanusuru na kila aina ya majanga.

"Kwa wazazi wenzangu, nawasihi msijisahau na tafrija na sherehe za sikukuu ni vyema mkatumia muda huu kuwaandaa watoto wetu kukabiliana na changamoto mpya za kimasomo, na kuhakikisha kwamba hawaikosi fursa adhimu ya elimu bila malipo inayotolewa na serikali yao,"

**SHIDA, MAFANIKIO 2021**

Awali, Rais Samia alibainisha vikwazo na mafanikio ya nchi kwa mwaka 2021, akikumbusha namna nchi ilivyokumbwa na mfumuko wa bei, janga la UVIKO-19 ilivyopoteza viongozi wa kitaifa wakiwamo Rais Dk. John Magufuli na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Maalim Seif Sharif Hamad.

Mbali na vikwazo hivyo, Rais alitaja mafanikio ya nchi katika mwaka huo yakijumuisha kudumisha amani na utulivu wa nchi, ukuaji chanya wa uchumi, Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi 11 zilizokua kiuchumi kati ya nchi 54 za Afrika licha ya mlipuko wa UVIKO-19, na kuhakikisha nchi ina akiba ya kutosheleza ya fedha za kigeni.

Vilevile, kuvutia uwekezaji na kurudisha fedha kwenye mzunguko kwa kufanya marekebisho mbalimbali ya kisera, kisheria, kikodi na kiutendaji.

"Matokeo yake tumeweza kuvutia uwekezaji kutoka miradi 186 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 1.013 mwaka 2020 hadi miradi 237 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 4.144 mwaka 2021," alibainisha.

Hata hivyo, Rais alikiri Sekta ya Utalii iliathiriwa kwa kiwango na UVIKO-19 na hatua mbalimbali za kuinusuru sekta hii kutodidimia zilichukuliwa na kuhakikisha sekta inarudi kwenye nafasi yake ya kuchangia uchumi wa nchi.

"Hadi mwezi Desemba mwaka 2021, sekta hii imeweza kujikongoja na kuingiza nchini watalii 1,400,000 kulinganishwa na watalii 620,867 kwa kipindi cha mwaka 2020, sawa na ongezeko la watalii 779,133. Matarajio yetu ni kushuhudia kukua zaidi kwa sekta hii kuanzia msimu wa 2022 na kuendelea," alisema.

Rais alitaja mafanikio mengine ni serikali kuendelea na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati, ikiwamo mradi wa ufuaji umeme wa Bwala la Nyerere, upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi, Daraja la Tanzanite, upanuzi wa barabara za viwanja vya ndege na ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

"Vilevile, katika kuhakikisha kwamba kunakuwa na mazingira mazuri ya kisiasa, Baraza la Vyama vya Siasa Tanzania limekutana na wadau mbalimbali wa siasa na demokrasia na kujadili kwa pamoja mustakabali na namna bora ya uendeshaji wa siasa za vyama vingi nchini kwetu.

"Matumaini yangu ni kwamba kikosi kazi kilichoundwa na Msajili wa Vyama vya Siasa, kitafanyia kazi maazimio ya mkutano huo kwa weledi. Serikali itapokea mapendekezo yatakayoletwa na tuone hatua za kuchukua ili tuweze kusonga mbele kwa pamoja kama taifa," alisema.

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE ULEMAVU**

## TAARIFA KWA UMMA

**WITO KWA VYUO NA TAASISI ZA MAFUNZO KUSHIRIKIANA NA SERIKALI KUTOA MAFUNZO YA UANAGENZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

1.0. Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu inatekeleza Programu ya Kukuza Ujuzi Nchini. Utekelezaji wa Programu hii umegawanyika katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni: Mafunzo ya Uanagenzi; Mafunzo ya kuongeza Ujuzi kwa Wafanyakazi; Mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu wa vyuo; na Kurasimisha Ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa Mafunzo. Lengo kuu la mafunzo ni kusaidia vijana kuwa na Ujuzi wa kuwawezesha kushindana katika soko la ajira la ndani na nje ya nchi pamoja na kuongeza wigo mpana wa kujiajiri au kuajiriwa.

2.0. Katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 kuanzia Januari 2022, Ofisi ya Waziri Mkuu imepanga kutoa mafunzo ya Uanagenzi kwa Vijana katika fani mbalimbali ili kuwawezesha kujiajiri na kuajiriwa. Mafunzo yatatolewa kwa vijana wa kitanzania wenye umri usiozidi miaka 35 na yatakuwa ya muda wa miezi Sita (6) darasani na miezi miwili mahala pa kazi.

3.0 Sifa za Vyuo na Taasisi kushiriki kutoa Mafunzo:

a) Vyuo vilivyosajiliwa na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) au Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) vyenye Daraja A au B au C;
b) Vyuo na taasisi zenye uwezo wa kutoa mafunzo kwa fani husika kuanzia wanafunzi 100 na kuendelea;
c) Vyuo vyenye Wakufunzi walioajiriwa na Chuo husika na wanatambulika na Mamlaka Serikali;
d) Vyuo vyenye miundombinu bora ikijumuisha karakana, mitambo na nyenzo za kufundishia na kujifunzia; na
e) Vyuo vyenye uzoefu usiopungua miaka mitano (5) na vimetoa mafunzo husika mfululizo.

4.0. Vyuo vyenye sifa za kutoa Mafunzo vinashauriwa kuwasilisha maombi ya kutoa Mafunzo husika kwa utaratibu ufuatao:

a) Barua ya kuomba kutoa mafunzo ikiainisha fani zitakazotolewa na idadi ya wanafunzi kwa fani;
b) Sifa za wakufunzi watakaotoa mafunzo (CV) kwa fani;
c) Muda wa kutoa mafunzo kwa fani;
d) Cheti cha usajili wa chuo;
e) Cheti cha mlipa Kodi (Tax Identification Number);
f) Gharama za kutoa mafunzo kwa fani na kwa mwanafunzi; na
g) Maelezo mengine ya ziada kadiri itakavyofaa.

5.0. Vyuo na Taasisi zitakazo wasilisha maombi zitafanyiwa upekuzi kuona kama zina uwezo wa kutoa mafunzo husika. Vyuo na Taasisi zitakazokidhi vigezo zitaitwa kwa majadiliano na Serikali kuhusu namna bora ya kushirikiana kutoa mafunzo husika.

6.0. Vyuo na Taasisi zinazopenda kushiriki kutoa mafunzo viwasilishe maombi kwa Katibu wa Bodi ya Ununuzi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, S. L. P. 980, DODOMA, Mtaa wa Reli. Maombi yawasilishwe kabla ya tarehe 15 Januari, 2022 saa 9.00 Alasiri.

**Imetolewa na:**
**KATIBU MKUU**

HABARI KITAIFA

# Adaiwa kumuua mume kwa maji moto, petroli

**Na Elisante John,** SINGIDA

MWALIMU wa Shule ya Sekondari Kinqmbeu, Iramba mkoani Singida, Simon Anthony (33), anadaiwa kuuawa na mkewe kwa kumwagiwa maji ya moto kisha kumwagiwa petroli na kuwashiwa kiberiti.

Anthony anadaiwa kufanyiwa unyama huo na mkewe Mwanaisha Shamir (29) nyumbani kwao Lulumba, mjini Kiomboi Desemba 27, 2021 majira ya saa 5:00 usiku.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Mutabihirwa, alisema chanzo cha mauaji hayo ni wivu wa mapenzi. Alisema mwanamke alikuwa akimtuhumu mumewe kuwa na uhusiano na wanawake wengine nje ya ndoa.

Licha ya kusababisha mauti ya mumewe aliyefia papo hapo kutokana na kuungua moto, mlipuko huo ulimrudia pia mwanamke huyo na kumjeruhi vibaya katika sehemu mbalimbali za mwili wake.

Aidha wakati moto ukishika kasi ndani ya chumba, pia ulisababisha watoto wawili wa wanandoa hao kujeruhiwa vibaya, Clara Simon wa miaka saba na Wisley Simon. Wengine ni mdogo wa marehemu, Apolinary Anthony (18), aliyejeruhiwa na moto wakati akijaribu kuwaokoa waathirika wa tukio hilo.

Kitendo hicho, Kamanda Mutabihirwa alisema kina viashiria vyote vya wivu wa mapenzi lakini akaitaka jamii kusuluhisha changamoto zao za ndoa kupitia kwa viongozi wa dini, mila au vyombo vya sheria badala ya kutumia njia za mkato, ikiwamo kukatisha uhai.

Mutabihirwa alibainisha kuwa, mwanamke huyo ingawa bado amelazwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida, anashikiliwa na Jeshi la Polisi ili achukuliwe hatua za kisheria.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga Adam Malima akizungumza na Meneja wa Wakala wa Maji na Mazingira Vijijini Upendo Lugongo (katikati) wakati wa utiaji saini mikataba 16 ya miradi ya maji itakayotekelezwa katika wilaya 7 za mkoa huo wenye thamani ya shilingi bilioni 8 Kushoto ni Katibu Tawala wa mkoa wa Tanga Pili Mnyema. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Waziri aitaka TANESCO kujitathmini utendaji

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NAIBU Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana na Ajira, Patrobas Katambi, amelitaka Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoani Shinyanga, kujitathimini kuhusu utendaji wake wa kazi.

Katambi amelitaka shirika hilo kufanya hivyo kutokana na kulalamikiwa na watu wengi kuhusu utoaji wa huduma mbovu.

Katambi ambaye ni Mbunge wa Shinyanga Mjini, alitoa kauli hiyo juzi kwenye kikao chake cha kusikiliza taarifa za utendaji kazi kwa mwaka uliopita kutoka taasisi mbalimbali za serikali.

Alisema amekuwa akipokea malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya utendaji kazi usioridhisha wa shirika hilo, ikiwamo kushindwa kuwaunganishia umeme kwa wakati licha ya kulipia huduma hiyo.

Malalamiko mengine, kwa mujibu wa Katambi, ni pamoja na kutofanya marekebisho ya ufungaji mita nzima baada ya kuzitoa mbovu licha ya kwamba wamekuwa wakitembea nazo kwenye magari.

"Malalamiko ya kukatika katika kwa umeme hilo tatizo nalifahamu ni la nchi nzima. Kunafanyika maboresho ya vifaa lakini hili la kuchelewa kuunganisha huduma za umeme kwa wananchi limekuwa sugu.

Naombeni mjitathimini na kama mnashindwa kufanya kazi nimwambie Waziri wa Nishati atutafutie watu sahihi," alisema Katambi.

"Taarifa zenu pia za kufungia watu huduma ya umeme zinachanganya. Juzi nilipofanya mkutano wa hadhara, Kaimu Meneja alisema mna wateja 900 wa kuwafungia umeme na kila siku mnafungia wateja 40. Wewe Meneja unasema mna wateja 3,000. hapa mkweli nani sasa?" alihoji Katambi.

Naibu Waziri alilitaka shirika hilo kuongeza ufanisi wa utendaji kazi badala ya kusukumwa au hadi kupewa maagizo na viongozi. Fanyeni kazi kwa kufuata miongozo na kuhudumia wananchi bila kujali matabaka," alisisitiza.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, alisema shirika hilo ni kikwazo mjini hapa na kwamba huduma zao ni mbovu na ni waongo.

Alisema hata taarifa zao wanazozitoa kwenye kikao cha Naibu Waziri Katambi zinatofautiana na zile ambazo waliziwasilisha kwenye kikao cha Baraza la Madiwani, na kuonyesha jinsi gani walivyo wababaishaji.

Diwani wa Kizumbi, Lubeni Kitinya, alisema baadhi ya watumishi wa shirika hilo wamekuwa wakiendekeza rushwa ndipo watoe huduma na kwamba kuna baadhi ya watu wana zaidi ya miezi sita tangu walipie huduma ya kufungiwa umeme lakini hawajafungiwa na mita ikiharibika wanatembea nayo kwenye magari hadi wapewe pesa.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Grace Ntungi, alisema maelekezo na ushauri ambao wamepewa wataufanyia kazi.

Awali, akiwasilisha taarifa yake alitaja miradi ya usambazaji umeme ambayo wanaitekeleza mkoani hapa kwa mwaka wa fedha 2021/22 kuwa ni 74 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.8.

# TV na king'amuzi vyampeleka jela

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Mkwajuni, Mchinga mkoani Lindi, Hamza Mchangampya (22), amehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka mitatu jela baada ya kupatikana na hatia ya kuvunja na kuiba mali zenye thamani ya Sh, 390,000, mali za Nasiri Liparapi.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Lindi, Consolata Singano, baada ya kuridhishwa pasipo shaka na ushahidi uliotolewa na upande wa mashitaka.

Kabla ya kutolewa kwa hukumu hiyo, Hakimu Singano alimwuliza mshtakiwa kama anazo sababu za msingi zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kwa kosa linalomkabili, hivyo kudai ni mkosaji wa mara ya kwanza na alifanya hivyo kwa madai ya ugumu wa maisha, hivyo apunguziwe adhabu.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Singano alimwuliza Mwanasheria wa Serikali, Godfrey Mramba, iwapo anazo kumbukumbu za makosa ya zamani kwa mshtakiwa na kujibu hana.

Hata hivyo, aliiomba mahakama kumpatia mshtakiwa adhabu kali ili iwe fundisho kwa wengine na kupunguza vitendo vya wizi.

Hakimu Singano alimhukumu mshtakiwa kupitia vifungu vya Sheria namba 265 na 258 (1) vya Kanuni ya adhabu Sura ya 16 Rejeo la 2019 kuhusu kosa la kuvunja, kutumikia kifungo cha mwaka mmoja gerezani, wakati la pili la kuiba kifungo cha miaka miwili.

Mwanzoni, ilidaiwa mbele ya mahakama hiyo kwamba Agosti 28, mwaka jana katika kijiji cha Mkwajuni, mshtakiwa alivunja nyumba ya Nasiri Lipalapi na kuiba vitu mbambali na kutoweka navyo.

Vitu hivyo vilitajwa kuwa ni televisheni moja yenye thamani ya Sh. 170,000, Decoder ya Azam Sh. 180,000, Flash disk ya Sh. 20,000 kebo ya waya yenye thamani ya Sh. 15,000, hivyo kufanya vyote kuwa na thamani ya Sh. 385,000.



Mwenyekiti wa Taasisi inayojishughulisha na huduma kwa watoto mapacha ya Eden Twins Foundation, Diana Mbena akiwa na mapacha watatu nyumbani kwao Buguruni Malapa, jijini Dar es Salaam alipokwenda kuwapa msaada wa chakula mwanzoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Dk. Mwinyi asisitiza kazi, mapambano dhidi ya rushwa, corona mwaka 2022

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema katika Mwaka Mpya wa 2022, wananchi waelekeze nguvu zaidi katika kufanya kazi pamoja na kupambana na ugonjwa wa UVIKO- 19.

Pia amesema mapambano dhidi ya rushwa na ubadhirifu wa mali ya uma yataendelezwa kwa nguvu zote huku akisisitiza kwamba watakaojihusisha na vitendo hivyo watachukuliwa hatua za kinidhamu na kisheria.

"Tuendelee kufanya kazi kwa bidii katika mwaka 2022 huku tukichukua tahadhari ya maradhi ya UVIKO - 19 hasa kwa kujikinga na aina mpya ya virusi vinavyojulikana kwa jina la Omicron ambavyo viliripotiwa kuwapo nchini Afrika Kusini tangu Novemba 24, 2021 na hivi sasa vimeenea katika nchi mbalimbali," alisema Dk. Mwinyi jana katika salamu zake za kuukaribisha Mwaka Mpya.

Alisema katika juhudi za kukabiliana na athari za kiuchumi zilizosababishwa na UVIKO - 19, serikali imepata mkopo wa dola za Kimarekani milioni 100 (Sh. bilioni 230 za Kitanzania).

Alisema janga la UVIKO- 19 lilikuwa changamoto kubwa ambalo Zanzibar, Tanzania na dunia nzima iliendelea kukabiliana nalo kwa mwaka 2021 na kwamba limechangia kwa kiasi kikubwa kuzorotesha uchumi kama ilivyo katika mataifa mbalimbali duniani.

Katika kukabiliana na janga hilo, alisema serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na ugonjwa huo kwa kushirikiana na taasisi za kimataifa, nchi marafiki, sekta binafsi na watumishi wa sekta ya afya.

Kuhusu mapambano dhidi ya rushwa, alisema serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria watu wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo bila muhali wala kumuonea huruma mtu yeyote.

"Nachukua fursa hii kuwahimiza wananchi tuendelee kushirikiana katika mapambano dhidi ya vitendo vya rushwa na ubadhirifu wa mali za umma, vitendo vya udhalilishaji pamoja na matumizi ya dawa za kulevya," alisema.

Hata hivyo, alisisitiza kuwa katika kupambana na vitendo hivyo, sheria zinapaswa kufuatwa ili kulinda haki za raia kwa mujibu wa Katiba.

"Nchi yetu inaongozwa kwa misingi ya haki na utawala bora. Kwa hivyo lazima sheria iwe inachukua mkondo wake na kuhakikisha tunalinda haki za kila raia kwa mujibu wa Katiba," alisema.

Kuhusu mwaka 2021, Dk. Mwinyi alisema nchi imeendelea kuwa na amani na utulivu pamoja na mshikamano vilivyoiwezesha serikali kutekeleza vyema majukumu yake kuwahudumia wananchi kukuza uchumi, kuimarisha miundombinu mbalimbali na kuendelea kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Pia alisema katika mwaka uliopita Tanzania imeweka historia kwa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa mwanamke wa kwanza kushika wadhifa huo, tangu Uhuru pamoja na Muungano wa Tanzania na Zanzibar. Hatua hiyo, alisema imeifanya kuwa moja ya nchi chache barani Afrika kuweka historia hiyo.

Pamoja na mambo hayo, alisema Tanzania ilikumbwa na misiba ya viongozi wakuu wa kiserikali wakiwamo Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli aliyefariki dunia Machi 17, 2021 na Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar.

# CRDB yaanza mwaka 2022 kivingine

**Na Rose Jacob,** MWANZA

BENKI ya CRDB imewakumbuka waumini wa dini ya Kiislamu kwa kuanzisha mikopo isiyo na riba wala makato yoyote katika akaunti mbalimbali zinazopatikana katika taasisi hiyo.

Kaimu Meneja wa CRDB Kanda ya Ziwa, Japhary Hassanali, alisema kanuni ya dini hiyo inaelekeza kuwa muumini wa Kiislamu akikopa na kulipa riba au kufanya jambo lolote kwa kutoa riba atakuwa ametenda dhambi, hivyo kuwafanya wengi kushindwa kukopa fedha kwa ajili ya kuendesha miradi yao.

"CRDB inatambua kuwa kuna wenzetu wa dini ya Kiislamu, wamekuwa hawapendi kutumia huduma za kibenki kutokana na kuwapo kwa riba, hivyo tumeanzisha huduma iitwayo Allbarak inayoanza mwaka huu wa 2022 inayolenga imani hiyo nchini kote ili wenzetu watumie fursa za kifedha,"alisema Hassanali. Pia alisema CRDB ina uwezo mkubwa wa kukopesha, hivyo wananchi waitumie vizuri elimu ya uchukuaji wa fedha, wasikope tu bali wakope wanapohitaji pesa kwa ajili kuweka kwenye mitaji yao. Lengo kubwa ni kuhakikisha miradi inakuwa mikubwa na kutoa huduma nzuri kwa wateja wao.

"Kwa mwaka 2021 wateja wapya waliofungua akaunti katika mikoa ya Kanda ya Ziwa ni 122,000. Tumeingia mkataba na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa abiria kupata huduma ya kukata tiketi za ndege popote walipo kupitia mtandao wa 'simbanking' bila kufika ofisini," alisema.

Meneja huyo pia alisema CRDB imeboresha huduma zake kupitia njia mbadala ambapo mtu yoyote anaweza kufanya miamala kwenye ATM hata kama hana akaunti ya CRDB ili mradi awe na uwezo wa kifedha kwenye simu, mfano M-Pesa, Tigo Pesa na atachukua fedha kwa kutumia namba yake ya siri.

Pia alisema kuna punguzo la asilimia tano hadi 10 kwa kadri mteja anapofanya miamala.

Baadhi ya waumini wa Kiislamu waliishukuru CRDB kwa kuliona hilo kwa kuwa wengi miongoni mwao walishindwa kutumia huduma za kibenki kutokana na maelekezo ya dini kuwa riba ni haramu kwa mwislamu.

"Sisi wajasiriamali wa Kiislamu tulikuwa tunapata tabu sana ya kukuza mitaji yetu kutokana na sehemu yoyote unayotaka mkopo lazima urejeshe na riba, jambo ambalo katika imani yetu ni haramu. Tunaipongeza CRDB kwa kuliona hilo," alisema Karima Juma mkazi wa Igoma jijini hapa.

# Bashungwa kicheko ujenzi wa madarasa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa amewapongeza viongozi wa serikali wilayani Karagwe kwa usimamizi thabiti wa Sh. bilioni 1.7 zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kupitia mpango wa UVIKO-19.

Pongezi za Waziri Bashungwa zinatokana na kukamilika kwa ujenzi wa vyumba 80 vya madarasa kwa zaidi ya asilimia 95 katika wilaya hiyo kabla ya kuanza kwa muhula mpya wa masomo kwa mwaka 2022.

Bashubgwa ambaye nui Mbunge wa Karagwe, juzi alielezea furaha yake kuona matokeo chanya yaliyotarajiwa yakitimia kwa wakati kutokana na ushirikiano mkubwa kati ya viongozi wa ngazi za shina, vijiji, kata hadi wilaya pamoja na wananchi kwa ujumla.

Alimshukuru pia Rais Samia kwa kutoa fedha nyingi za maendeleo hasa kwa ajili ya kujenga na kuboresha miundombinu mbalimbali katika wilaya ya Karagwe kama vile barabara, maji, afya pamoja na mikopo ya vijana na wanawake.

Kuhusu uboreshaji wa kahawa, Waziri Bashungwa alisema licha ya serikali kuimarisha ushirika pia imeruhusu wanunuzi binafsi ili kuongeza ushindani wa bei na hamasa kwa wakulima kuendelea kulima zao hilo kutokana na mafanikio ya moja kwa moja wanayoyapata.

Katika ziara hiyo, Waziri Bashungwa alizitembelea kata za Igurwa, Nyakabanga na Chonyonyo na kukutana na viongozi wa mashina na matawi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) pamoja na watumishi wa serikali na kusikiliza maoni na matamanio yao pamoja na kuwatakia heri ya Sikukuu za Krisimasi na Mwaka Mpya.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mwaka 2022 ulete mabadiliko kwa wanamichezo na wasanii

**LEO** ni Sikukuu ya Mwaka Mpya. Ni siku ya kwanza ya mwaka 2022. Mhariri na wafanyakazi wote wa gazeti la Nipashe wanapenda kuwatakia kila la kheri na mafanikio wasomaji wa gazeti hili la kila siku la Nipashe. Tunauanza mwaka 2022 huku Watanzania tukiwa chini ya Rais, Samia Suluhu Hassan. Ndio kiongozi wetu mkuu. Tunamwombea afya njema na mafanikio katika uongozi wake.

Kama ambavyo kila taasisi au kampuni huwa na malengo yake ya kila mwaka, ni vyema pia wanamichezo na wasanii wakawa na mipango ambayo inahitaji kufikia mafanikio.

Ili ufikie mafanikio yoyote, ni vyema kuandaa mikakati ya kukufikisha huko ambapo unahitaji. Mara nyingi mafanikio au matarajio ambayo huwekwa kwenye mikakati huwa ni chanya.

Tunawakumbusha huu ni mwanzo wa mwaka na ndio wakati mzuri wa kila mmoja kujiwekea malengo na hatimaye inapofika mwisho wa mwaka, unakamilisha hesabu.

Kwa wanamichezo, huu ni wakati mzuri wa kila mmoja kujiwekea utaratibu wa kuona nini anahitaji kukipata kwa mwaka huu. Unapokuwa na mikakati, ni rahisi kutembelea mikakati yako na hatimaye unapata wepesi wa kufikia malengo.

Ni ngumu kupata mafanikio kwa mtu, timu, klabu, chama, taasisi au kampuni kupata mafanikio hali ya kuwa huko nyuma hakukuwa na mipango au malengo ambayo yangekupelekea kupata matokeo chanya.

Tusidanganyike, hakuna mafanikio ambayo yanaweza kupatikana kwa miujiza. Huu ndio wakati sahihi wa kila mwanamichezo au msanii kujiwekea mikakati ya wapi anahitaji kufika ndani ya mwaka huu 2022. Unapofanya hivyo, inakusaidia 'kucheza' kwenye eneo sahihi na si vinginevyo. Mwanamichezo au msanii mwenye malengo hujiweka katika nafasi nzuri ya kutimiza ndoto zake ukilinganisha na yule ambaye hakuwa na mipango yoyote tangu mwaka ulipoanza mpaka pale miezi itakapoendelea kuyoyoma.

Ni wazi na ukweli usiofichika msanii au mwanamichezo ambaye atajiandaa mapema na vizuri kwa ajili ya kushiriki mashindano mbalimbali ya ndani au nje ya nchi yake, atakuwa ni mwenye kutarajia kuvuna matunda na si yule ambaye anasubiri muda wa mashindano ukaribie ndipo aanze maandalizi ya 'zimamoto'.

Tukumbuke kufanya maandalizi au kuwa na mipango ndio kuwekeza. Mwanamichezo au msanii ambaye hajawekeza vizuri nguvu na akili zake katika shughuli ambayo anaifanya asitarajie kuvuna kikubwa, tubadilike kama kweli tunataka kuona wanamichezo wetu wanafika mbali, wanashiriki mashindano makubwa na kurejea nyumbani na medali za dhahabu.


Rais Samia alishaweka wazi anahitaji kuona heshima ya Tanzania kufanya vyema katika mashindano mbalimbali inarejea, lakini hili litaonekana pale wahusika watakapokuwa tayari kuwasilisha mapema programu na kalenda za michuano wanayotarajia kushiriki katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kusaidiwa maandalizi.

Wale wanaocheza soka tunasema pia bado hawajachelewa, hiki ni kipindi cha dirisha dogo la usajili. Ni nafasi ya timu kurekebisha mapungufu waliyoyabaini kwenye mechi 10 walizocheza na hatimaye vikosi vyao kuimarika na kuwa tayari kukamilisha msimu huu kwa kishindo.

Ni mapema kukata tamaa, hata kwa timu zile zilizoko mkiani katika msimamo wa ligi, tunawakumbusha lolote linaweza kutokea endapo watatumia vyema dirisha dogo kuongeza wachezaji ambao watawasaidia kwenye vikosi vyao na hatimaye kumaliza ngwe ya mwisho wakiwa imara. Tunawakumbusha ili ndoto za mafanikio zitimie, ni vyema wanamichezo na wasanii wetu wakaweka mbele nidhamu binafsi wakati wote wanapokuwa kambini au nyumbani ili kulinda viwango vyao.

Nidhamu ni siri kubwa kwa mwanamichezo au msanii kupata mafanikio. Unaweza kuwa na kipaji cha kuimba, kucheza ngoma au kusakata kandanda, lakini kama nidhamu yako ni mbovu, hakuna lolote ambalo unaweza kufanikiwa kwa sababu ya nidhamu mbovu utakayokuwa nayo mwanamichezo mwenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Waamuzi ukaribisheni 2022 kwa uamuzi sahihi, haki

Na Adam Fungamwango

**MWAKA** 2021 ambao umetamatika jana ulikuwa wa mafanikio makubwa kwenye soka la Tanzania kwa mambo mengi.

Ni mwaka ambao pamoja na kwamba timu yetu ya taifa, Taifa Stars haikufanya vyema sana kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa, lakini angalau mashabiki wa soka wameridhishwa na viwango vya wachezaji.

Ilikuwa ni bahati mbaya tu kwa Stars kushindwa kutinga michuano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022), itakayoanza kutimua vumbi Januari 6, mwaka huu nchini Cameroon, lakini pia kusonga mbele kwenye kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kucheza fainali zijazo za Kombe la Dunia zitakazofanyika Qatar.

Ni mwaka ambao tumeshuhudia Taifa Stars ikishinda ugenini na kutoka sare, tena ya wageni kulazimisha.

Stars iliifunga Benin, na kutoka sare dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), ikiwa ugenini. Kilichoiponza Stars ni kushindwa tu kuutumia vyema uwanja wa nyumbani, Benjamin Mkapa. Kama ingeweza kuutumia, saa hizi ingekuwa ipo Cameroon katika AFCON, na pia ingekuwa moja kati ya timu 10 zitakazocheza hatua ya mtoano kusaka timu zitakazoshiriki Kombe la Dunia.

Kwenye michuano ya soka la wanawake, Twiga Stars, na Tanzanite zimefanya vizuri na kuiletea nchi sifa na vikombe pia.

Timu ya taifa ya walemavu ikafanikiwa kutinga fainali za Kombe la Dunia la michuano hiyo inayotarajiwa kuchezwa nchini Uturuki.

Kwenye ngazi ya klabu, Simba ilifika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na kutolewa dhidi ya Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini, mechi ya kwanza ikichapwa mabao 4-0, Mei 15, mwaka jana nchini Afrika Kusini na licha ya kushinda mabao 3-0, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam hayakutosha kuwafanya wasonge mbele, lakini ilikuwa ni hatua kubwa ambayo ilisababisha Tanzania kupata tena nafasi nne za kuiwakilisha nchi katika michuano ya kimataifa licha ya kutotumika vizuri.

Pamoja na kwamba, Simba mwaka huu, haikuingia kwenye hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, na timu za Tanzania kama Yanga, Azam na Biashara United kushindwa kusonga mbele, lakini Simba imeingia hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho, ambapo itacheza hatua hiyo mwaka huu.

Shirikisho la Soka Nchini (TFF), nalo halikuwa nyuma kwani limejitahidi sana kutafuta wadhamini kiasi cha kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara kuwa bora mno msimu huu.

Klabu nazo zimejitahidi sana kutengeneza vikosi bora, kupambana na kutoa upinzani mkali. Ndiyo maana si ajabu kwenye Ligi Kuu timu ikashinda ugenini, tofauti na zamani.

Cha kusikitisha ni kwamba sehemu pekee ambayo inaonekana haijajirekebisha ni waamuzi. Timu zimekuwa bora, wachezaji wanaonekana wana viwango vya hali ya juu, lakini baadhi ya waamuzi wameonekana si bora na hawaendani na kasi ya soka linavyoonekana kukua na kuwa na thamani nchini.

Baadhi ya waamuzi wameonekana kuwa ni waamuzi wa matokeo, badala ya waamuzi wa mchezo.

Wamekuwa na baadhi ya maamuzi yanayotia shaka. Wameonekana kuamua matukio hasa ya penalti zenye utata, kiasi cha kuwafanya baadhi ya mashabiki kuamini huenda ndiyo sababu inayowafanya wasichaguliwe kuchezesha fainali ya AFCON, ukimwondoa, Frank Komba.

Kumekuwa na malalamiko makubwa kwa waamuzi wa sasa kwenye soka la Tanzania kuliko eneo lingine. Inavyoonekana TFF, Bodi ya Ligi na Chama cha Waamuzi Nchini (FRAT), wana kazi kubwa ya kufanya kuboresha eneo hilo kwa manufaa ya soka la taifa letu.

Angalau tuanze kuona mwaka huu wa 2022 wimbo wa waamuzi uanze kupungua. Makosa ya kibinadamu yapo na hata mashabiki wanajua, lakini mengine yanaonekana kabisa yana utata.

Kiongozi wa zamani wa Yanga na Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba hivi majuzi alisema isidhaniwe mashabiki wanaokwenda kutazama soka hawajui sheria za soka na kuwataka wachezeshe kwa haki ili kuufanya mchezo wa soka kuwa wa kuvutia na usio na matokeo yanayofahamika.

Mwaka 2022, uwe mwaka wa waamuzi kubadilika na kujisafisha na tuhuma zinazoelekezwa kwao mara kwa mara.

# Fedha za UVIKO- 19 zapunguza msongamano wanafunzi darasani

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

UJENZI wa vyumba saba vya madarasa vilivyojengwa kwa fedha za UVIKO - 19 na nguvu ya wananchi, umepunguza msongamano darasani kutoka wanafunzi 70 hadi wastani wa wanafunzi 40 na 45.

Nafuu hiyo imebainika katika Shule ya Sekondari ya Tunamkumbuka iliyoko katika kata ya Butelankuzi Wilaya ya Bukoba, mkoani Kagera.

Akitoa taarifa kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Murshid Ngeze, aliyefika kukagua ujenzi wa madarasa hayo, Mkuu wa Shule, Robert Kasaju, alisema walipokea Sh. milioni 80 ambazo ni fedha za UVIKO - 19 ambazo zimetumika kujenga vyumba vinne vya madarasa na kutengeneza madawati 200.

"Lakini pia wananchi wa kata ya Butelankuzi walichangia nguvu zao zenye thamani ya karibia Sh. milioni 18 na kujenga vyumba vingine vitatu vya madarasa hadi hatua ya maboma.

"Kutokana na kazi hiyo, Halmashauri iliongeza Sh. milioni 37.5 kwa ajili ya ukamilishaji. Hatua hii imesaidia kupunguza msongamano darasani na sasa walimu wanaweza kufundisha kwa uhuru na kuwezesha wanafunzi kuelewa vizuri," alisema Kasaju.

Alisema kabla ya kupata madarasa hayo, walikuwa na vyumba 12 vya madarasa ambavyo vilitumiwa na wanafunzi 762 na kwamba sasa wamefikisha vyumba vya madarasa 19.

"Kuna wakati wazazi walikuwa wakisuasua kuleta watoto shuleni wakihofia kuambiwa kuchangia fedha kwa ajili ya madawati lakini sasa mtoto anavaa sare yake ya shule, anabeba madaftari yake anakuja anaingia darasani bila hofu ya mzazi wake kuombwa chochote.

Tunaishukuru sana serikali kwa kutupatia fedha hizi," alisema.

Akizungumza baada ya kukagua ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule mbalimbali, Ngeze alisema walipokea Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 85 vya madarasa na kutengeneza madawati 4,250.

"Kila kata ilipata mgawo wa madarasa mpaka sasa yamekamilika kwa asilimia 98, hivyo ni maeneo machache ya ukamilishaji yaliyobaki ambayo kufikia tarehe za mwanzoni mwa Januari yatakuwa yamekamilishwa kwa ajili ya kupokea wanafunzi 7,017 wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2022," alisema Ngeze.



Wananchi wa kata ya Songa, wilayani Muheza, mkoani Tanga, wakishiriki nguvu kazi katika ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa katika shule ya sekondari ya kata hiyo juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Moto wateketeza nyumba mama lishe

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa kijiji cha Mungurumo, kata ya Liwale Mjini mkoani Lindi, Asia Njikatile, anahifadhiwa na majirani baada ya nyumba aliyokuwa akiishi kuteketea kwa moto alipokuwa ndani amelala na familia yake.

Hata hivyo, bado hasara iliyopatikana kutokana na moto huo haijafahamika mara moja.

Taarifa kutoka wilayani humo na kuthibitishwa na mamlaka za serikali, mhusika na majirani, zinaeleza moto huo ulitokea Desemba 28, mwaka huu, saa 4:00 usiku eneo la nyuma ya nyumba hiyo.

Akithibitisha tukio hilo kupitia simu yake ya mkononi, Njikatile alisema ni kweli amekutwa na tatizo hilo kwa nyumba yake kuungua moto akiwa ndani amelala na familia yake.

Siku hiyo ya tukio majira ya 3:00 usiku, alisema alirejea kutoka sokoni anakofanyia shughuli za kuuza chakula (mama lishe) na kukuta mazingira ya nyumba yake yakiwa salama, hivyo kuingia ndani na kulala.

Alisema muda si mrefu alisikia sauti za watu zikiita moto moto, hali iliyomsukuma atoke ndani ya nyumba ili kufahamu kinachoendelea na pia kuungana na wenzake kusaidia kudhibiti tukio husika. "Nilipotoka nje ili kufahamu kinachoendelea nikaona ni nyumba yangu ndiyo inayoungua moto na kuanza kuuzima," alisema Njikatile.

Alisema katika jitihada hizo, walichofanikiwa kuokoa ni upande mmoja wa kitenge alichokuwa amevaa mwilini wakati anatoka ndani na baiskeli moja, huku vitu na bidhaa mbalimbali vikiwamo vyakula vikiteketea kwa moto. Njikatile ametaja vitu vilivyoteketea ni vitanda vya kulalia vitatu na magodoro, mabegi ya nguo matatu, mtambo mmoja wa sola wenye thamani ya Sh. milioni 1.2 magunia matatu ya mahindi, viroba sita vya unga wa sembe na ngano, televisheni, sabufa na vitu vingine vya matumizi ya ndani.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mungurumo, Kassim Ngatawile na majirani, Ramadhani Nassoro na Mtandumbache Ally, walisema moto huo ulitokea upande wa nyuma ya nyumba hiyo na kwamba chanzo halisi hakijafahamika mara moja.

Walisema kwa sasa Njikatile anahifadhiwa na majirani huku wananchi wakiendelea na jitihada za kumjengea nyumba ya miti ili kujihifadhi na familia yake pamoja na mama yake mzazi anayeishi naye. Pia walitoa wito wananchi wengine kumsaidia mama huyo.

# Ulinzi waimarishwa Mwaka Mpya Dar

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam limejipanga kikamilifu kuhakikisha usalama unaimarika na kuzuia vitendo vya kihalifu na vya uvunjaji wa amani katika Sikukuu za Mwaka Mpya.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Kamanda wa Polisi wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi (ACP) Jumanne Muliro, alisema wameweka doria katika maeneo mbalimbali ambayo yatakuwa na mikusanyiko ya watu.

"Jeshi la Polisi Kanda Maalumu limejipanga kikamilifu katika kuhakikisha mifumo ya kuzuia vitendo vya kihalifu inasimamiwa vizuri ikiwa ni pamoja na doria na misako katika maeneo yote ya nyumba za ibada, kumbi za starehe na kwenye fukwe ili wananchi washerehekee Mwaka Mpya kwa amani na utulivu," alisema Muliro.

Aliongeza kwa kutoa tahadhari kwa mtu au kikundi cha watu chenye lengo la kufanya vitendo vya kihalifu kutojihusisha na matendo hayo maovu.

Pia alishauri wananchi kuhakikisha mtu mmoja au zaidi anabaki kwenye makazi wakati wa kwenda kwenye matembezi au ibada na kuepuka kuendesha magari wakiwa wametumia vileo. Alisema madereva watakaotiliwa shaka watapimwa na watakaobainika watachukuliwa hatua.

Kamanda pia aliwataka madereva wa magari, bajaji na pikipiki na watumiaji wengine wa barabara kuzingatia sheria na taratibu za usalama barabarani na kuepuka kuharibu miundombinu kwa kigezo cha kusherekea.

Muliro pia aliwataka wananchi kutoa taarifa za uhalifu na wahalifu uliopo katika maeneo yanayowazunguka katika kituo chochote cha Polisi au kwa kupiga simu namba 111/112.

# Kafulila: Si hiari watoto kuanza shule

**Na Happy Severine,** BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, amewaagiza wakuu wa wilaya zote mkoani hapa kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kuanza shule wanapelekwa kuanza na jambo hilo si hiari.

Kafulila alitoa agizo hilo jana wakati akipokea madarasa 449 ya UVIKO -19 kutoka kwa wakuu wa wilaya na kuelekeza kuwa watoto wote wenye umri wa kwenda shuleni ni lazima waende.

"Wakuu wa wilaya baada ya ujenzi wa madarasa haya ya UVIKO-19 kukamilika kwa asilimia 100 mkoa mzima, sasa hakikisheni wanafunzi wote ambao wanatakiwa kwenda kuanza shule wanapelekwa kuanza," amesema.

"Wazazi na walezi wanatakiwa kuelewa kuwa kupeleka mtoto shule si hiari bali ni lazima na kama serikali lazima tusimamie hilo. Wakuu wa wilaya hakikisheni hakuna mtoto atakayeshindwa kuanza shule, iwe ya awali (chekechea), msingi au sekondari kidato cha kwanza," alisisitiza.

Kuhusu ujenzi wa madarasa hayo, Kafulila alisema mkoa wa Simiyu ulipewa Sh. bilioni 8.9 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 449 yakiwamo 380 ya sekondari na 69 ya shule shikizi.

Alisema ujenzi wa madarasa hayo yote umekamilika na mkoa uko tayari kwa ajili ya kupokea wanafunzi wote ambao watatakiwa kuanza shule. Alizipongeza kamati zote zilizohusika kusimamia ujenzi huo.

"Nizipongeze kamati zote ambazo zimehusika katika ujenzi wa madarasa haya. Mmefanya kazi kubwa sana na tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa fedha hizi ambazo zimewezesha ujenzi wa madarasa yote haya," alisema Kafulila.

Kiongozi huyo pia aliwataka wananchi kwenye maeneo ambako madarasa hayo yamejengwa, kuhakikisha wanayatunza na kuyatumia kwa kazi iliyokusudiwa huku akiwataka waone kama zawadi kutoka kwa Rais.

"Kimsingi kama Rais asingelifanya hivi, wananchi sasa hivi mngelikuwa mnaangaika kujenga madarasa, lakini kwa fedha hizi hamjatoa mchango wowote, na muda huu mnautumia kwa ajili ya maendeleo yenu, lazima tumpongeze Rias wetu na kumshukuru," amesema Kafulila.

Malimbo Buhalata, mkazi wa mtaa wa Sina alisema wanamshukuru Rais kwa kuwajengea vyumba hivyo vya madarasa kwa kuwa awali watoto wao walikuwa wakitembea umbali wa kilometa sita kwenda mpaka shule mama.

Alisema kwa sasa watoto wao watapunguza kuchoka kutokana na kutembea umbali mrefu na kuwahi shuleni kwa ajili ya kupata vipindi kwa wakati.



Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Dk.Richard Masika, (kulia), akimsikiliza Mhandisi wa Umeme wa Taasisi hiyo, Anasai Mathew, wakati wa hafla ya uzinduzi wa bodi ya (DIT ICB), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Iringa yazindua mpango afya maendeleo kwa vijana balehe

**Na Steven William,** IRINGA

WILAYA ya Iringa imezindua kampeni ya kitaifa ya ajenda ya kuwekeza katika afya na maendeleo kwa vijana balehe.

Kampeni hiyo kitaifa kwa wilaya ya Iringa ilizinduliwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo .

Akizungumza na wananchi katika uzinduzi huo, Moyo alisema mpango huo utasaidia kuwekeza katika afya ya maendeleo ya vijana balehe. Moyo alisema ajenda ya kuwekeza katika afya na maendeleo kwa kundi hilo ni mpango wa miaka minne kuanzia mwaka wa fedha wa 2021/12 hadi 2024/25.

Alisema ili kuhakikisha mpango huo unafanikiwa katika wilaya ya Iringa, lazima kuwe na mikakati ya pamoja kwa wadau wote wa mpango huo wa muda mrefu.

Moyo alisema kuwa anatambua changamoto za vijana balehe wana majaribu mengi na sasa kuanzisha mpango huo watapata elimu ambayo itawasaidia katika maisha yao. Aliwapongeza waandaaji wa ajenda ya kuwekeza afya ya maendeleo kwa vijana balehe jambo ambalo alisema ni kitu muhimu sana na kwamba anaunga mkono jambo hilo muhimu.

Katika hatua nyingine, Moyo aliwakumbusha vijana na wazee kwenda kupata chanjo ya kinga ya virusi vya corona huku akisisitiza kuwa haina madhara yoyote.

Alisema viongozi wote wa nchi wamepata chanjo wakiongozwa na Rais Samia Suluhu lakini mpaka sasa hawajapata madhara yoyote, hivyo kuthibitisha kuwa chanjo hiyo ni salama.

Naye mkazi wa manispaa ya Iringa, Charles Mhilu, alisema chanjo ni kitu muhimu ndiyo maana imekuwa ikisisitizwa na viongozi mbalimbali akiwamo mkuu wa wilaya ya Iringa.

# Ulingo yasisitiza usawa wa kijinsia

**Na Maulid Mmbaga**

UMOJA wa Vyama vya Wanawake Wanasiasa Tanzania (Ulingo) umesema kuanzia leo utaanza mkakati wa utoaji wa elimu kwa Watanzania ili kuielimisha jamii juu ya masuala ya usawa wa kijinsia na demokrasia.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam, Mratibu wa Taifa wa Ulingo, Dk. Ave-Maria Semakafu, alisema wamefikia hatua hiyo ili kuiongezea uelewa jamii juu ya umuhimu wa kuzingatia usawa wa kijinsia na kuepusha ukatili dhidi ya wanawake.

Pia alisema wameamua kulitekeleza hilo baada ya kubaini uwapo wa unyanyasaji wa viongozi wanawake katika ngazi za utoaji wa uamuzi huku akieleza kutiwa shaka na baadhi ya kauli za viongozi ambazo kwa mtazamo wake alitafsiri kama unyanyasaji wa kijinsia.

"Tunalaani vitendo vya unyanyasaji dhidi ya wanawake. Kuanzia Januari Mosi (leo) tutaingia darasani na yoyote atakayehusika na unyanyasaji dhidi ya wanawake hatutamnyamazia tena na tutamshughulikia. Sisi wanawake tunasema kutozingatia usawa wa kijinsia ni udhalilishaji," alisema Dk. Semakafu.

Aliongeza kuwa jukumu lao ni kuhakikisha usawa wa kijinsia unazingatiwa nchini, kuufanya uongozi wa kisiasa kuwa na sura ya kitaifa pamoja na kukemea unyanyapaa unaoifanya Tanzania ikaonekana ina unyanyasaji katika demokrasia.

Dk. Semakafu pia alisema mara kwa mara wamekuwa wakizungumzia unyanyasaji wa wanawake viongozi ndani ya vyama vya siasa, nyakati za uchaguzi wakiwa kama viongozi na wapigakura. Alisema kwa sasa suala hilo limejitokeza kwa kiasi kikubwa.

Pia alitoa wito kwa viongozi na Watanzania kwa ujumla kupuuza wale wote wanaokuja na nia ya kudhalilisha utu wa wanawake, huku akisisitiza kuwa utu utawale kwa manufaa ya taifa na wananchi.



# Viongozi waonywa kutumia corona mtaji kisiasa, kidini

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama cha Wakulima (AAFP), Rashid Rai, amewataka viongozi wa siasa na dini kutoutumia ugonjwa wa corona katika harakati za kiasisa na kidini.

Pia amewataka viongozi wa vyama vya siasa kuondokana na fikra potofu na badala yake waiunge mkono serikali katika juhudi zake za kutoa elimu na kuwafikia Watanzania ili kushiriki kikamilifu chanjo ya ugonjwa huo.

Rai alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa kata ya Makole. Mtaa wa Chadulu pamoja na viongozi wa chama hicho jijini hapa kwa ajili ya kuwahamasisha kujitokeza kwa wingi kushiriki chanjo dhidi ya corona.

Alisema bado kuna baadhi ya viongozi wa kisiasa na dini wanaokwamisha harakati za serikali katika kuhakikisha watu wake wanapatiwa chanjo hiyo ili kujilinda dhidi ya maradhi hayo.

Ugonjwa huo, alisema usifananishwe na usiingizwe kwenye siasa au dini, bali kinachotakiwa ni kuhakikisha viongozi wanashirikiana na serikali katika kuwahamasisha watu kujitokeza kwa hiari ili kufanikisha azma hiyo muhimu katika kujilinda.

Viongozi wa vyama vya siasa na dini, alisema wana nafasi kubwa katika kuhamasisha watu wao kushiriki chanjo ambayo serikali imegharimia mamilioni ya fedha kwa ajili ya Watanzania kuwawezesha kupata chanjo hiyo bure.

Alisema bado kwa upande wa viongozi wa siasa na dini jambo hili hawajaitikia vya kutosha hivyo alitoa wito kwa watanzania kujitokeza kwa hiari kuchanja ili kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan ambaye ameonyesha mfano wa kuchanja.

Alisema Rais Samia alionyesha njia kuwaongoza Watanzania, hivyo viongozi wa siasa na dini hata na wale wa serikali washiriki kikamilifu kuwahamasisha watu wachanje kwa faida yao.

Mwenyekiti wa Vijana wa Chama hicho, Mark Mhemela, aliwahamasisha vijana kuwa mstari wa mbele kujitokeza ili kushiriki chanjo hiyo kwa maendeleo ya afya zao.

Pia aliwataka vijana kuondokana na propaganda na taarifa zinazotolewa zisizo za kweli ambazo zinapotosha kuhusiana na kirusi kilichoibuka badala yake wajitokeze kwa wingi ili kuchanja kwa lengo la kujilinda na corona.

Alisema kirusi kilichoibuka hivi karibuni hakichagui kama kilichokuwa kimejitokeza hapo mwanzo, hivyo vijana wanatakiwa kumuunga mkono rais ikizingatiwa kuwa wao ndiyo nguvu kazi ya taifa hili.

## Bashe ataja sababu umaskini wakulima

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amesema wakulima wa Tanzania ni maskini kutokana na mifumo iliyotengenezwa na vyama vya ushirika kutowawezesha kufanya kilimo kibiashara.

Bashe pia aliwataka viongozi wa ushirika kusimamia wakulima kulima mazao ya kimkakati ya muda mfupi kukabiliana na changamoto za kifedha pindi mazao ya msimu yanapoisha.

Akizungumza na vyama vya ushirika hivi karibuni jijini hapa, Bashe alisema mkulima kuwa na zao moja kwa mwaka mzima kumepitwa na wakati kwa kuwa huwasababishia kuwa maskini baada ya msimu wa mazao kuisha.

"Mkulima kuwa na zao moja mwaka mzima ni ushamba, lakini ukimwezesha kulima mazao ya muda mfupi hata kwa ekari moja kwenye shamba lake la mazao ya muda mrefu mkulima huyo mwezi wa nane atakuwa na kipato na Januari atakuwa na kipato," alisema.

Bashe alisema kasi ya kulima mazao hayo ndio itakayosaidia kuinua hali za wakulima nchini kwani inawasaidia kulima mazao ya muda mfupi kwa pamoja.

"Na mimi naamini kwamba kweli wakulima ni maskini lakini si maskini kwa kutaka bali ni kwa mifumo waliyotengenezewa na vyama vya ushirika," alisema.

Kuhusu mauzo ya mwaka 2021, Bashe alisema amefurahishwa na uuzaji wa mazao kwa uhalali yakiwemo pamba na korosho kwani hakuna malalamiko yoyote yaliyomfikia.

Naibu Mrajisi wa Vyama vya Ushirika, Charles Malunde, alivitaka vyama vya ushirika nchini kufanyia kazi maagizo yanayotolewa na Wizara ya Kilimo ili kufanya kilimo chenye tija.



Noel Mwalimu (kulia) akimpamba kwa kumwekea urembo Mzee Musa Lemugoha (kushoto) ikiwa ni sehemu ya mila na desturi za kabila la Wagogo kama walivyokutwa kijiji cha Nzali Wilaya Chamwino Mkoani Dodoma jana, **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Tani milioni 1.3 chakula kuzalishwa 2021/22

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA msimu wa kilimo wa mwaka 2021/22 mkoa wa Dodoma umelenga kulima hekta 751,259 za mazao ya chakula na 540,482 za mazao ya biashara.

Pia mpango huo una lengo la kuzalisha tani 1,349,147.82 na tani 596,338.7 za mazao ya chakula na biashara mtawalia.

Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Dodoma, Bernard Abraham, alibainisha hayo juzi alipokuwa akiwasilisha taarifa ya idara yake kwenye kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema mkoa unakadiriwa kuwa na watu 2,729,668 na mahitaji ya chakula ni tani 647,614 za chakula cha wanga na tani 97,142.06 ni mahitaji ya chakula cha utomwili.

"Takwimu za mavuno zinaonyesha mkoa umevuna tani 898,583 za mazao ya wanga na tani 72,477 za mazao ya utomwili," alisema Abraham.

Alisema kwa msingi huo, mkoa unajitosheleza kwa mazao ya wanga na kuwa na ziada ya tani 250,969 na utakuwa na upungufu wa tani 24,665 za vyakula vya utomwili.

Kadhalika, alizitaja changamoto katika sekta ya kilimo kwa mkoa wa Dodoma ni pamoja na matumizi hafifu ya pembejeo na zana bora.

"Wakulima kutozingatia kanuni bora za kilimo katika shughuli zao za uzalishaji mazao, wananchi wengi kutokuwa na tabia ya kuhifadhi chakula cha kutosha kwa matumizi ya muda mrefu," alisema Abraham.

Changamoto nyingine alisema ni masoko yasiyokuwa ya uhakika na bei ndogo kwa mazao ya kilimo pamoja na mabadiliko tabianchi yanayosababisha ukame na milipuko ya visumbufu vya mimea.

Kadhalika aliibainisha mikakati ya kutatua changamoto hizo ikiwa ni pamoja na kusimamia uzalishaji wa mazao ya kipaumbele ambayo ni mtama, alizeti na zabibu. Mkakati mwingine ni ushiriki wa viongozi katika kusimamia kilimo, kuimarisha mawasilino ili kufikisha huduma kwa wakulima.

"Lakini pia mikakati mingine ni pamoja na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa," alisisitiza.



# SMZ yaeleza azma kuifanya Mji Mkongwe urithi wa dunia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale imesema itaendelea kusimamia dhamira ya serikali ya kuubakisha Mji Mkongwe katika urithi wa dunia.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Wizara hiyo, Lela Muhamed Mussa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya wizara yake katika miaka 58 ya Mapinduzi.

Alisema kuendelea kubaki kwa Mji Mkongwe katika urithi wa dunia, inaufanya kuwa moja ya vivutio vikubwa vya wageni wanaotembelea Zanzibar.

Lela alisema wizara yake itahakikisha majengo yaliyomo ndani ya Mji Mkongwe yanafanyiwa matengenezo kwa mujibu wa mpango mkuu wa uhifadhi.

"Wizara itahakikisha inaendeleza juhudi za kuyahifadhi, kuyalinda na kuyatunza maeneo na majengo ya kihistoria yaliyopo nchini kwa lengo la kurudisha uasili wa maeneo hayo,"alisema Waziri Lela.

Pia alisema mikakati ya wizara hiyo ni kuendelea kufanya mazungumzo na mawakala wanaoleta watalii kwa lengo la kuongeza idadi ya wageni watakaotembelea Zanzibar.

Alisema pia watashirikiana kwa karibu na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) katika kuwatafuta wawekezaji kwa lengo la kuwekeza katika sekta ya utalii na mambo ya kale.

Kwa mujibu wa Lela, wizara itaendelea kushiriki katika maonyesho na makongamano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa lengo la kuitangaza Zanzibar na kuibua fursa za uwekezaji.

Katika hatua nyingine Waziri aliwataka wananchi waliovamia maeneo ya kihistoria kuanza utaratibu wa kuhama katika maeneo hayo.

"Tunafahamu kwamba baadhi ya maeneo mengi ya kihistoria yako pembezoni mwa fukwe za bahari, hivyo wakati wa kuongezeka kwa kina cha maji ya bahari inasababisha athari kwa maeneo ya majengo ya historia," alisema.




Madereva wa bodaboda, wakisubiri taa ziwaruhusu kuvuka barabara ya Bogamoyo eneo la ITV Manispaa ya Kinondoni Dar es Salaam, juzi huku wakiwa wamevuka alama za pundamilia. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Uwazi kusisitizwa mipango ya uchumi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Rais Fedha na Mipango imesema itaendeleza uwazi katika mipango yote ya kiuchumi inayohusu fedha za umma ili kuhakikisha kila mwananchi anafahamu hatua zinzoendelea ndani ya serikali.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Fedha na Mipango ambaye pia Mwenyekiti Jukwaa la Uchumi wa Bajeti, Dk. Juma Malik Akil, aliyasema hayo jana wakati akifungua jukwaa la uchumi na bajeti kwa serikali kuu na serikali za mitaa lililofanyika kwenye ukumbi wa Sheikh Idrissa Abdul Wakil, Kikwajuni.

Alisema hatua hiyo itasaidia wananchi kuondoa wasiwasi na serikali na kuendelea kuiamini katika kupanga mipango yake mbalimbali ya maendeleo.

Pia alisema lengo la jukwaa hilo kushirikisha wadau mbalimbali ambao watachangia kwa kutoa mawazo yao katika maendeleo na kuona hawamuachi mtu nyuma katika jambo hilo.

Matayarisho na utekelezaji wa jukwaa la uchumi, alisema vinalenga kukidhi matakwa ya sheria na kuendelea na harakati za matayarisho kwa bajeti ya mwaka 2022/23 pamoja na mapitio ya muda wa kati ambayo itaendelea hadi mwaka 2025 kwa utaratibu uliozoeleka.

Alisema ni kawaida kwa serikali kushirikisha wadau na wananchi katika majukwaa kama hayo ambayo yanatoa fursa watu kutoa maoni yao katika kuboresha jambo hilo

Kuhusu changamoto ya UVIKO-19, alisema mbali na mikakati hiyo, Zanzibar kama zilivyo nchi zingine duniani, imechukua tahadhari na mipango katika uchumi wake kutokana na athari za maradhi hayo.

Alisema ni vyema wanapopanga bajeti hiyo kutengeneza njia ambazo zitasaidia kutekeleza bajeti hiyo huku wakiendelea kukabiliana na changamoto hiyo ambayo inaendelea kuathiri dunia.

Hata hivyo alibainisha kuwa uchumi wa Zanzibar unategemewa kukua kwa takriban asilimia 5.9 pamoja na kuwa na mtikisiko wa maradhi ya UVIKO- 19.

Kamishana wa Bajeti Ofisi ya Rais Fedha na Mipango, Saumu Khatib Haji, alisema matarajio ni kuona wanapomaliza mwaka huu wanatekeleza bajeti hiyo vizuri.

# Mbunge ahimiza utunzaji miundombinu ya maji

**Na Mwandishi Wetu**

MBUNGE wa Mwera, Zahour Mohamed Haji, amewataka wananchi kuhifadhi na kulinda miundombinu ya maji ili idumu kwa muda mrefu na kusaidia jamii.

Kauli hiyo aliitoa jana Mtoni Kidatu, Chemchem Wilaya ya Magharibi "A" Unguja wakati wa uzinduzi wa mradi wa maji safi na salama baada ya kufanyiwa matengenezo makubwa.

Alisema ushirikiano unahitajika katika kuitunza miundombinu hiyo ili lengo la serikali kuwaondolea usumbufu wananchi wake kufanikiwa.

Lengo la kuzindua mradi huo, alisema ni kuwasaidia wananchi hasa kinamama ambao walikuwa na kilio cha muda mrefu na kwamba jambo hilo ni moja ya ahadi alizozitoa na kuzitekeleza .

Alisema ataendelea kutoa huduma mbalimbali za kijamii ambazo zimekuwa kero kubwa ikiwamo utengenezaji wa miundombinu ya barabara, kuwapatia mtaji, mafunzo na masoko wajasiriamali wadogo ili kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao.

Pia alisema katika jitihada za kutatua kero zilizopo anatarajia kuongeza mashine za kusukumia maji ili zirahisishe kusambaza huduma hiyo kwa haraka na kuahidi kutoa Sh. 340,000 kila mwezi kwa ajili ya gharama za umeme.

Hata hivyo, aliitaka kamati ya kusimamia maji kufanya matengenezo kila panapoharibika ili kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo kwa wananchi.

"Serikali haitaki ubaguzi, hivyo ni marufuku kujitokeza mtu kujimilikisha mradi huu," alisema.

Katibu wa Kamati ya Mradi wa kisima hicho, Mohamed Ali Juma, alimpongeza mbunge huyo kwa kuwapatia huduma hiyo ambayo waliikosa kwa miaka sita.

Alisema ameahidi kushirikiana na wanakamati wenzake ili kuhakikisha huduma hiyo inadumu na kuwasaidia wananchi wa Mwera hadi Mtoni Kidatu.

Naye Asha Mohamed Khatib kutoka shehia ya Mtoni Kidatu Chemchem, alimshukuru Mbunge huyo kwa niaba ya wanawake wenzake kwa kuwatua ndoo kichwani na kuwaondolea usumbufu wa ukosefu wa huduma hiyo.

Aliwataka wananchi wenzake kutoa ushirikiano kwa kuchangia mambo madogo yanapohitajika ili kukiwezesha kisima hicho kiwe endelevu kisaidie na vizazi vijavyo.



DWAYNE AKATAA DILI NONO

Ukurasa.14

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
JUMAMOSI JANUARI 1, 2022



## MWAKA WA USHINDANI

# Diamond, Harmonize watunishiana misuli

MWAKA 2021 umekuwa wa mafanikio katika tasnia ya muziki nchini. Lakini ndani ya mafanikio hayo kumekuwa na mikiki mikiki ambayo iliwaacha baadhi ya wasanii katika tafrani na wengine kupoteza mwelekeo.

Jambo ambalo litakumbukwa na wengi ni kufika kilele cha mgogoro uliokuwa ukifukuta kati ya wana muziki wawili nyota,Diamond Platnumz na Harmonize.

Mgogoro huo ambao ulianza chini kwa chini ulipaliliwa baada ya kujiondoa kwa Harmonize katika lebo ya WCB na kisha kuanzisha lebo yake ya Konde Gang, ambayo inafanya vizuri.

Ndani ya mwaka huo mvutano mkali, majivuno na majigambo zilitawala pande zote mbili, huku ikirembeshwa na maneno ya kukejeliana kutoka kwa wapambe wa wasanii hao.

Wakati bifu hilo linazidi kushika kasi, Harmonize aliamua kutumbua nyongo kwa kueleza kile anachodai kufanyiwa na Diamond, wakati uhusiano wao ulipokatika ghafla ndani ya WCB.

Harmonize aliamua kuweka wazi kwamba yeye anakuwa muhanga wa wivu, umbea na fitna za watu wanaomzunguka Diamond, kiasi ambacho aliaminishwa kwamba yeye yupo katika harakati ya kumpindua kisanii.

Hapo ndipo dunia ilipofahamu kwamba kuna mambo mengi zaidi ya hayo, lakini Harmonize alishindwa kuyasema, labda aliona siku ya kufanya hivyo bado haijafika.

Watu walianza kupata ukweli angalau kwa upande mmoja, kwani Diamond hakutaka kunyanyua mdomo wake kuzungumzia hilo, alikaa kimya akiamini kuwa ni busara kukaa kimya ili kupisha upepo upite na kazi iendelee.

Wasanii hao wameingia mwaka 2022 wakiwa bado wanaangaliana jicho pembe, kila mmoja akitaka Mungu amnyoshee mkono na kumfungulia milango zaidi ya mafanikio.

Matumaini ya mashabiki wengi wa muziki ni kuona wanamuziki hao wanatumia mwaka 2022 kuwa wa mapatano na kuonyeshana upendo.

Hata hivyo, macho ya wengi ni kusubiri kuona kama wasanii hao watautumia mwaka huu kuwa wa kupata suluhu kwa maslahi ya muziki wa Bongo Fleva na nchi kwa ujumla.

BASI SAWA

## Ukiona hawaeleweki wapunguze

WASANII wawili wameingia mwaka 2022 wakiwa na kauli mbiu ya kupunguza watu wasio na msaada katika orodha ya marafiki.

Mwanamuziki wa Bongo Fleva, Tundaman alianza kusema kupitia Instagrama kwamba kama una rafiki snitch, mpenda bata, miyeyusho au humuelewi we mpunguze tu, huu ndio mtindo wa 2022.

Naye Irene Uwoya kupitia ukurasa wake wa Instagram amekubaliana na kauli hiyo kwa kueleza mwaka huu ni wa kupunguza orodha ya watu.

"Mwakani ni mwaka wa kupunguza watu, #2022punguzawatu".



## Ney mbona mtata hivyo?




RAPA mwenye mitizamo tata, Ney wa Mitego, amesema wanaume wanaowaacha wapenzi wao, waache tabia ya kulalamika pale wanapoona kuna mtu kajitokeza kumuhudumia.

Wanasema ushemeji huwa haufi lakini sio kwa msanii Ney wa Mitego ambaye anasema hana ushemeji kama mkali wa muziki wa singeli Manfongo.

Kupitia EATV, Ney amesema ikitokea mtu au mshkaji wake ameachana na mpenzi wake, halafu yeye akampenda basi anamchukua na wasilaumiane katika hilo.

"Tusilaumiane kama umemuacha mwanamke na mimi nikamtokea hiyo itakuwa haki yangu, nina wajibu wa kuishi naye," amesema.



## Amapiano wazidi kuwavuruga

MJADALA wa muziki wa Amapiano ambao asili yake ni kutoka Afrika Kusini umezidi kushika kasi na kusababisha wasanii wa Bongo Fleva kugawanyika mara mbili kimtazamo.

Baadhi ya wanamuziki kama Ali Kiba na Maua Sama, wametoa kauli zao kuwa kamwe hawataingia katika kundi la wasanii wanaopenda muziki huo hata kama mashabiki wanaonekana kuupenda.

Barnaba kwa upande wake, ameeleza kuwa hakuna tishio la Amapiano kuididimiza Bongo Fleva, kutokana na miziki hiyo kuwa tofauti.

"Nadhani bado Bongo Flavor ina nguvu sana kuliko Amapino kingine lazima watu wajue Amapiano sio aina ya muziki, bali kwa lugha rahisi ni mchanganyiko wa mapigo ya Dj wa Afrika Kusini," amesema.



## AliKiba kuanza 2022 kipekee

MWAKA 2022 umeanza kwa neema kwa mwanamuziki nyota Alikiba, kwani amejipanga kuachia albam yake mpya.

Kupitia akaunti yake ya twitter Alikiba ameandika kwamba "Nafikiria kuachia Album nyingine 2022".

Ikumbukwe kwamba Oktoba 7, 2021 Alikiba aliachia Album yake ya tatu 'Only One King' ikiwa na ngoma 16 ambayo inaendelea kufanya vizuri kwenye uwanja wa muziki.

## I think i hate my wife; Kosea kupanda basi, sio mke

**Na Adam Fungamwango**

KUNA msemo unaosema kosea vitu vyote duniani, lakini usikosee kuoa au kuolewa. Msemo huu una maana kuwa ukikosea kumpata mwenza, basi utakuwa na matatizo makubwa kwenye maisha yako.

Ni kwa sababu mke au mume ni mtu wa karibu mno ambaye unaishi naye kila siku na mko naye muda mrefu mno kuliko ndugu zako.

Binadamu akishakuwa mtu mzima huacha kuishi na ndugu zake na kuanza kuishi na mtu mwingine kabisa ambaye naye ametoka kwingine. Inafaa umpate mtu ambaye utaishi naye kwa hali ya upendo, furaha na amani, lakini ikiwa kinyume chake ni mateso makubwa.

Ndiyo maana tunafundishwa kuwa makini mno kwenye kuchagua mke au kumfahamu vizuri mwanaume unayekwenda kuishi naye. Hii imeonekana kwenye filamu ya 'I think i hate my wife', aliyekutana na mwanamke tu barabarani bila kumfahamu vizuri, baadaye akamgeuza kuwa mkewe, alivyopata tabu na mateso.

Imechezwa na Simom Mwapagatwa maarufu kama 'Rado', Jacob Steven 'JB', Shamsa Ford, na wengineo.

Rado akiwa ndani ya gari yake, akakutana na msichana anayeonekana anahitaji msaada wa lifti, lakini pia anaonekana si mwenyeji wa jiji la Dar. Anampeleka nyumbani kwake. Awali alionekana kumsaidia kama mfanyakazi wa ndani, lakini kadri siku zilivyozidi kusonga mbele, ndipo alipouona uzuri wa msichana huyo. Akaamua kumuoa awe mkewe. Usilolijua ni kama usiku wa kiza, kumbe mwanamke yule ni mtoto wa mjini aliyekuwa akifanya kazi kwenye majumba ya starehe jijini.

Pia mwanamke huyo alikuwa na mambo ya kishirikina. Alimtengeneza Rado hakufurukuta. Akawa sasa anafanya kila anachoambiwa na mkewe Shamsa. Mamilioni ya pesa yanahamishwa kwenye akaunti yake na siku chache baadaye, watu wanavamia nyumbani kwake, wakitaka atoe hati ya nyumba.

Kumbe yale yote yako nyuma ya mkewe Shamsa. Mikasa iliyompata, ilimfanya Rado awe kichaa. JB ambaye alikuwa rafiki yake na alikuwa akifanya naye kazi, alimtafuta na alipompata akamhamishia nyumbani kwake, huku akimuuguza. Akapona, lakini akaanza na moja. Rado akawa kwenye mahusiano mengine na mpwa wa rafiki yake JB kwa sababu ndiye aliyekuwa naye karibu akimfariji.

Rado, mkewe mpya, JB na mkewe waliamua kwenda kwa Mchungaji kwa sababu Shamsa alionekana bado anawafuatilia kwa nguvu za kishirikina. Mchungaji anavunja nguvu za kishetani, Rado anaanza maisha mapya na mke mwingine.






## Kali tano za Defao zilizobamba Bongo

**Na Adam Fungamwango**

ZILIKUWA zimesalia siku tatu tu afikishe siku yake ya kuzaliwa. Si mwingine ni mwanamuziki bora na maarufu Afrika, raia wa Jamhuri ya Kidemkokrasi ya Congo, General Defao.

Jina lake kamili ni Matumona Defao Lulendo ambaye alifariki Jumatatu iliyopita nchini Cameroon baada ya kuugua kwa muda mfupi.

Hata hivyo, baadhi ya ndugu zake na jamaa wa karibu wanasema mkali huyo alikuwa anasumbuliwa na ugonjwa wa kisukari kwa muda mrefu na alifariki kwenye Hospitali ya Laquintinie jijini Douala alikokwenda kwenye shughuli zake za muziki. Inadaiwa pia kuwa ugonjwa aliokuwa nao ulimchachamalia baada ya kuathiriwa na virusi vya COVID-19.

Kifo cha Defao kimeleta vilio na simanzi kubwa kwa wapenzi na mashabiki wa muziki huo duniani kote, ikiwemo nchini Tanzania.

Wapenzi wa muziki wa Tanzania wanamkumbuka sana, kwani si mara moja wala mbili au tatu alishawahi kuja nchini kwa ziara ya kimuziki.

Alikuwa ni mwanamuziki ambae hakuwa tu na uwezo wa kutunga na kuimba nyimbo nzuri, lakini alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza na kulishambulia jukwaa.

Nyimbo za mwanamuziki huyo ambaye kama ingefika Desemba 31 siku ya kuzaliwa kwake, angefikisha miaka 63. Alizaliwa terehe hiyo mwaka 1958, jijini Kinshasa.

Tuziangalie baadhi ya nyimbo zilizopata umaarufu mkubwa nchini Tanzania.

**Famille Kikuta**

Ni moja kati ya nyimbo zake bora kabisa na zilizopendwa sana nchini Tanzania. Kwenye sherehe hafla yoyote ilikuwa haiwezi kuisha kabla ya wimbo huu kupigwa.

'Famille Kikuta' ambayo kuna sehemu anaimba 'Okibinda nko nayo, okimi bana nayo..', umo kwenye albamu ya 'Pitie Mon Amour' aliyoitoa mwaka 1997.

**Animation**

Huu ulikuwa ni wimbo wa kuchezesha zaidi. Ukipigwa huu hakuna mtu aliyekuwa anakaa kwenye kiti. Wabongo waliobatiza jina lililotokana na maneno yaliyoimbwa kwenye nyimbo hiyo, wakayatengenezea maneno yao kwa kiswahili 'Mimi ni buzi eee nichune ee'. Ni wimbo uliokuwa kwenye albamu ya 'Sala Noki' ya mwaka 1997.

**Sala Noki**

Huu ni wimbo bora kabisa uliokuwa kwenye albamu yenye jina hilo. Ni wimbo ulioimbwa kwa hisia na vyombo vikapangiliwa vema, huku Defao na wenzake wakicheza kwa madaha, mbwembwe na ustadi. "Hatukusema Mamayae, hakusema kusanza.." ni moja kati ya maneno ya rap yaliyomo kwenye wimbo huo wa mwaka 1997.

**Nikusema Nikutaka**


'Nikusema Nikutaka' ni jina la albamu aliyoitoa mwaka 1998, akimshirikisha mwanamuziki na mfanyabiashara mkubwa nchini Zambia, Suke Chile.

Ni albamu iliyokuwa na mafanikio makubwa kwa sababu karibuni nyimbo zote 10 alizotoa zilikuwa moto wa kuotea mbali, ikiwemo uliobeba jina la albamu mwenyewe akiimba kwa hisia kali.

**Bibi yangu Hanitaki Tena**

"Bibi yangu hanitaki tena, anapenda mpaka bana Tanzania, Dar es Salaam."

Ni baadhi ya maneno yaliyokuwa kwenye wimbo huo ambao jina halisi unaitwa 'Mama Ministre' Umo kwenye albamu ya 'Nikusema Nikutaka' ya mwaka 1998. Ni wimbo uliotokea kupendwa sana na mashabiki nchini ambao waliubatiza jina la 'Bibi yangu Hanitaki Tena'.



# Dwayne akataa dili nono

Muigizaji Dwayne Johnson maarufu kama the "The Rock" amekataa ombi la kurejea kuigiza muendelezo wa filamu ya Fast & Furious sehemu ya 10.

Mwezi Novemba mwaka huu muigizaji Mark Sinclair "Vin Diesel" kupitia ukurasa wake wa instagram alimuomba The Rock arudi kumalizia sehemu ya mwisho ya Fast & Furious kwa ajili ya mashabiki wao na kutimiza ahadi yao kwa marehemu Paul Walker.

"Nilishangazwa sana na posti ile ya Vin Diesel, mwezi wa sita mwaka huu niliongea nae faragha na kumwambia sitaweza kuigiza tena filamu hiyo ila nitatoa ushirikiano wangu katika kuandaa filamu hiyo ili kuhakikisha inafanikiwa na hata washirki wengine wote niliongea nao na walinielewa." Amekiambia kituo cha CNN.



## Kanye West hataki kushindwa

RAPA maarufu wa Marekani, Kanye West, ameamua kununua jumba la kifahari karibu na mtaa anaoishi mke wake Kim Kardashian.

Kulingana na gazeti la DailyMail, mwanamuziki huyo bilionea amenunua nyumba hiyo yenye ukubwa wa futi 3651, kwa dola milioni 4.5 sawa na shilingi bilioni 10.4.

Nyumba hiyo ipo katika eneo lenye ukubwa wa heka 1.07, inaelezwa kuwa ya kifahari zaidi yenye vyumba vitano na vyoo vitano.

## Yul mengine umwachie mwenyewe

MWIGIZAJI nyota kutoka Nollywood, Yul Edochie, amemtaja mwanamuziki Shetta Wale kuwa mtu ambaye haheshimu wasanii kutoka nchini mwake.

Kulingana na maoni yake, Edochie, amesema kitendo cha kutoa ishara mbaya kwa watu anaopingana nao ni kitendo cha aibu na kukosa utu.

Katika tamasha la Uhuru lilofanyika katika uwanja wa michezo wa Accra nchini Ghana, alionyesha ishara ya kidole kama njia ya kuwanyamazisha wakosoaji wake.





## Dr Dre avunja benki kununua talaka

RAPA mkongwe wa Marekani, Dr. Dre amejikuta akivunja benki kwa ajili ya kumlipa fidia aliyekuwa mke wake, Nicole Young, baada ya kumpa talaka.

Kulingana na mtandao wa TMZ, Dre amekubali kulipa dola milioni 100 kama fidia sawa na shilingi bilioni 230.54.


Katika makubaliano hayo, Dre ataendelea kumiliki mali zingine kama majumba ya kifahari ya Malibu, Calabasas na nyumba nyingine iliyopo Los Angeles.

## Omondi anavyomkubali Diamond

MSANII wa vichekesho kutoka Kenya, Eric Omondi, amemtaja Diamond Platnumz na kundi la Sauti Soul, kuwa ni wanamuziki wenye mafanikio kwa Afrika Mashariki.

Amesema wasanii kutoka Afrika Magharibi wameonyesha uwezo wao mkubwa ikiwamo kushirikiana na wanamuziki wakubwa wa Marekani, lakini kwa Kenya mambo yamekuwa magumu.


"Mwanamuziki Pekee wa Afrika Mashariki ninayemkubali ni Diamond Platnumz (Tumpe sifa pale anapostahili Chibu anajaribu), Sauti sol wanajaribu lakini haitoshi" ameandika katika ukurasa wake wa Instagram.



# OMICRON YAMALIZA VIBAYA 2021

## •Dunia yatawala mashaka, hofu tupu
## •X-masi, Mwaka Mpya zakosa msisimko

**Na Mwandishi Wetu**



UNAWEZA kusema dunia imepigwa na tsunami ya Omicron. Wanasayansi, wanasiasa na watu wote wameingia mwaka 2022 wakiwa na hofu juu ya maisha yao.

Kama ilivyokuwa miaka miwili iliyopita baada ya kuibuka kwa mara ya kwanza virusi vya corona, watu duniani kote wamesherehekea Sikukuu muhimu za X-Mas na Mwaka Mpya wakiwa katika vikwazo vikali.

Kwa ujumla hakuna anayejua lini ugonjwa wa corona hasa virusi vipya vya Omicron vitaisha lini ili kuifanya dunia iwe sehemu salama ya kuishi.

Uwepo wa virusi hivyo vimesababisha mataifa ya ulaya, Marekani, Israel na nchi za Kiarabu, kuchukua hatua kali ya kudhibiti usambaaji wake ikiwamo kupiga marufuku safari za ndege kwenda katika baadhi ya nchi za Kiafrika.

Kirusi hicho kinachobadilika kwa haraka sana kiligunduliwa nchini Afrika Kusini mapema Novemba 2021 na kisha kuripotiwa kwa Shirika la Afya Duniani (WHO), kuwa ni ugonjwa unaoleta hofu.

Aina hiyo iligundulika katika jimbo lenye wakazi wengi zaidi la Afrika Kusini, Gauteng, na baadae kusambaa kwa kasi ya mwanga wa radi duniani kote.

Hata hivyo, WHO imeonya dhidi ya nchi zinazoweka vikwazo vya kusafiri kwa haraka, ikisema wanapaswa kuzingatia mbinu nzuri ya kupambana, lakini nchi nyingi zimezuia safari za anga ili kukabiliana na kirusi hicho.

Mkurugenzi wa Afrika wa WHO, Matshidiso Moeti, alionya zuio hilo linaweza kuleta madhara zaidi kuliko hatari iliyopo.

"Pamoja na aina hiyo ya Omicron sasa iliyogunduliwa katika maeneo kadhaa ya dunia, kuweka marufuku ya kusafiri ambayo inalenga Afrika inaathiri mshikamano wa kimataifa." Amesema.

### HAKUNA SHEREHE ZA X-MASI

Kama ilivyokuwa kawaida ya waumini wa Kikristo, sherehe za Krismasi zimekuwa muhimu kwao kwani zinawafanya jamii kuwa pamoja, kutembeleana na kupeana zawadi.

Katika mataifa ya Ulaya, katika kipindi hicho cha Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, mitaa inakuwa imebadilika kwa mapambo na taa za kila aina.

Lakini hali imekuwa tofauti, kwani watu wamesherehekea sikukuu hizo wakiwa majumbani kwao huku wakikabiliwa na masharti makali ya kutotembeleana yaliyowekwa na serikali zao.

Hali hiyo sawa na wimbi la kwanza lililoanza mwishoni mwa mwaka 2020, lilisababisha marufuku ya kutoka nje mwezi Novemba na muda mrefu katika Mwaka Mpya ulikuwa ukitumiwa kukaa ndani.

### HOFU TOFAUTI NA UHALISIA

Pamoja na watu kuwa na hofu, lakini imebainika mtu akipata Omicron, kuna uwezekano mdogo wa kuwa mgonjwa sana kuliko aina nyingine za virusi vya corona zilizopita.

Uchunguzi kutoka duniani kote unatoa taswira thabiti kwamba Omicron ni dhaifu kuliko virusi vya Delta, na uwezekano wa chini wa asilimia 30 hadi 70 ya watu walioambukizwa hawalazwi hospitalini.

Omicron inaweza kusababisha dalili za wakati wa baridi kama vile maumivu ya koo, mafua na maumivu ya kichwa, lakini hiyo haimaanishi kuwa hali itakuwa nyepesi kwa kila mtu.

### KUENEA KASI YA RADI

Kusambaa kwa kasi zaidi kuliko virusi vingine, inaweza kuongeza hofu kwamba inaweza isithibitiwe na baadhi ya chanjo ya kukinga mwili.

Uingereza ina viwango vya rekodi vya covid na kesi zilizothibitishwa mnamo mwezi Novemba pekee ilifikia 120,000, lakini idadi hiyo ni ndogo kutokana na wengi hawaendi hospitali.

Uingereza imeshuhudia wagonjwa wengi wa Omicron waliofika hospitalini wako chini ya umri wa miaka 40, kwa hivyo haijajulikana nini kitatokea wakati itafikia wazee na makundi ya watu wanaoishi na magonjwa ya muda mrefu.

Uwezo wa Omicron kukwepa kinga kwa sehemu inamaanisha kuwa kuna uwezekano wa watu wazee zaidi kuambukizwa kuliko wakati wa wimbi la Delta.

### MCHANGANYIKO WA DELTA, OMICRON

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO),Tedros Adhanom Ghebreyesus, ametaka kuwepo na tahadhari wakati dunia inapitia katika wimbi hilo.

Ufaransa iliripoti kuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wanaopata maambukizi, kila siku wanapata kesi 208,000.

Marekani imeripoti wastani wa kesi 265,427 kwa siku katika wiki iliyopita, kulingana na Johns Hopkins.

Poland iliripoti vifo 794 vinavyohusiana na Covid,idadi kubwa zaidi katika wimbi lake la nne la janga hilo. Zaidi ya robo tatu ya watu hao ni wale ambao hawajachanjwa.

Utafiti unaonyesha kuwa Omicroni dhaifu kuliko kirusi aina ya Delta, lakini inaambukiza zaidi. Walakini, Dk Tedros alionya ni "tishio pacha" la anuwai mbili ambazo ni sehemu ya mzigo wa jumla wa kesi.

Dk Anthony Fauci, mtaalamu mkuu wa magonjwa ya kuambukiza wa Marekani, ameiambia CNN kuwa maambukizi ya Omicron huenda yakafikia kilele mwishoni mwa Januari nchini Marekani, kwa kuzingatia idadi ya watu ya kiwango cha chanjo.

Mataifa kadhaa tajiri yamezindua mipango ya kuongeza dozi ya tatu ya chanjo ya Covid, ikiwa ni pamoja na Uingereza ambapo asilimia 57 ya watu zaidi ya miaka 12 sasa wamepata chanjo ya tatu.

Hata hivyo, Tedros aliwaambia waandishi wa habari kampeni kubwa nchi tajiri kutoa chanjo za ziada zina uwezekano wa kuongeza muda wa janga hili, kwani wanaelekeza vifaa kutoka kwa nchi masikini, ambazo hazina chanjo, na hivyo kuoa fursa zaidi kwa virusi kuenea na kubadilika.

Aliendelea kusema "kila mtu afanye azimio la Mwaka Mpya 2022 kuwa nyuma ya kampeni ya chanjo ya asilimia 70 ya ulimwengu ifikapo katikati ya 2022,"

Takriban nchi 100 bado hazijafikia lengo la awali la chanjo ya asilimia 40 watu wao.

Kulingana na ripoti ya WHO iliyochapishwa Jumanne, idadi ya maambukizo mapya ya Covid ya anuwai zote ilikua kwa 57% barani Ulaya katika wiki kabla ya 26 Desemba, na kwa 30% katika Amerika.




### AFRIKA YAONEWA

Rais Uhuru Kenyatta ametoa wito kwa mataifa ya Magharibi kutofunga mipaka yao kutokana na aina mpya ya corona Omicron.

Kauli hiyo inaonyesha viongozi wa Afrika kuchoshwa na tabia za mataifa tajiri kuchukua hatua tofauti na ile iliyochukuliwa China baada ya kugundulika kwa mara ya kwanza ugonjwa huo mwaka 2020.

"Usifunge mipaka, msitufungie tena jamani ..Hakuna mtu ambaye yuko salama na Covid, hadi tutakapokuwa salama sote," anasema rais Kenyatta.

"Covid-19 haitashindwa kwa kufunga nchi au kwa kufunga sehemu za ulimwengu ambazo tunadhani zina shida,"alisema.

Kuna orodha ndefu ya nchi zimefunga mipaka yao kwa eneo hilo tangu wanasayansi wa Afrika Kusini kutangaza aina mpya ya coronavirus wiki iliyopita.

Kusimamishwa ni kwa kuzingatia uamuzi wa serikali wa kupiga marufuku kwa muda mawasiliano ya anga kwenda Botswana, Eswatini, Lesotho, Msumbiji, Namibia, Afrika Kusini, Kenya, Tanzania, Ethiopia, Uganda na Zimbabwe.

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Ijue kanga, vazi rasmi lenye mafumbo, vijembe na maudhui ya WhatsApp leo hii

**Na Adam Fungamwango**

MAZUNGUMZO, malumbano, mabishano, vijembe na mada mbalimbali tunaziona leo kwenye mitandao ya kijamii kama vile 'whatsapp', 'instagram", facebook', 'twitter' yameanza mbali, maana staili zake, aina ya salamu za kupashana na vigezo vingine vingi, kanga zilitumika vilivyo.

Ndiyo maana misemo, namna ya mipashano, mawasiliano ya kijamii, kwa zama hizo, ambazo simu za mkononi hata kompyuta, si tu kwamba zilikuwa anasa tu, hata kuwepo kwake tulisikia hukooo, ughaibuni!

Ukitaka kujua mawasiliano ya kanga ambayo pia ni vazi rasmi yalivyonoga zama hizo, sogea ukapate makazi kwenye nyumba yenye wapangaji wengi na hasa maarufu 'vyumba sita' iwe pongezi, vijembe au vijambo vyovyote vile vya kiswahili, kanga inafanya kazi yake.

Usishangae mwanamama kutoka chumba kimoja, anapita na kanga yenye maandishi fulani kisha mwingine, mara tu baada ya kuangalia, unatoka msonyo huo 'chwaaaaa!' ambao kwa zama hizo lilikuwa ni tusi lisilo la tamko, lakini salamu kamili zinafika.

Kutokana na utandawazi kuzidi kukua, pamoja na kuingia kwa nguo nyingi kutoka nje ya nchi, maarufu kama mitumba, imeonekana kuua kwa kiasi kikubwa soko la nguo aina ya kanga.

Ni vazi lililokuwa likipendwa sana na kinamama, likivaliwa sehemu yoyote ile, iwe nyumbani, sokoni, wakati mwingine hata kama safarini au kutembelea ndugu.

Kilichokuwa kinatofautisha ni aina ya kanga tu. Kuna za nyumbani na za safari. Kwa sasa kuna matumizi madogo sana ya vazi hilo kwa miaka ya hivi karibuni. Ingawa wanawake bado wanaendelea kuvaa, lakini labda wakiwa nyumbani tu, tena si mara kwa mara, maana siku hizi madera nayo yameshika chati. Wanawake wanashinda na madera, kanga kama anakwenda sokoni, au sehemu yoyote itakuwa ni kama nguo ya akiba, itawekwa kwenye mkoba tu kwa ajili ya dharura na labda kwenye nyumba za uswahilini sana.

Zamani kanga lilikuwa ndiyo vazi rasmi namba moja kwa mtoto wa kike, ndiyo yatafuata mavazi mengine kama sketi, gauni na nguo zingine za kike zinazofanana na hizo.

Vilevile zamani vazi la kanga hasa kwa wakinamama kwa ukanda wa Pwani mbali na kuwa ni vazi zilikuwa na kazi yake nyingine. Ilikuwa ni kufikisha ujumbe, kukogana na wenzake kwa misemo, vijembe na mafumbo.




Hii ilikuwa zaidi kwa kinamama wa Dar es Salaam, Pwani, Tanga, na hata nje ya Tanzania, maeneo kama ya Mombasa. Ndiyo maana maeneo hayo yakawa na viwanda vya kutengenezea kanga kama Kiwanda cha Nguo cha Urafiki, Dar es Salaam na hata Mombasa kulikuwa na viwanda vilivyokuwa vikizalisha, zikawa maarufu nchini kama 'kanga za Mombasa'.

Wanawake waliokuwa wakiishi maeneo ya Ukanda wa Pwani miaka hiyo kuanzia 1960 na kuendelea, wawe wamezaliwa hapo, au kutoka bara na kuzoea mazingira, walikuwa hawashikiki kwa kupeana ujumbe mbalimbali uliokuwa unawasilishwa kwa nguo hizo.

Kanga zilikuwa zinaandikwa jumbe mbalimbali, ambazo kinamama walizitumia kununua ujumbe anaoutaka na kuvaa mpaka pale anayemkusudia aone.

Hakuwa wakigombana kwa maneno, na ambaye amevaliwa ujumbe huo, naye atatafuta pesa, au kumuomba mumewe pesa akanune kanga yenye maneno ya mafumbo ambayo yanamjibu yule aliyemvalia. Yaani ilikuwa ni kama taarabu tu. Huyu akimuwekea mwenzake wimbo huu, mwenzake naye ataujibu kwa wimbo huu.

Viwanda navyo vilijitahidi kwenda na soko, kubuni maneno au jumbe fulani, halafu baadaye wanatengeneza zenye majibu yake. Maneno ya kwenye kanga yalikuwa yanazaliwa kila kunapokucha kuendana na matukio kwenye jamii.

**Wanawake waliokuwa wakiishi maeneo ya Ukanda wa Pwani miaka hiyo kuanzia 1960 na kuendelea, wawe wamezaliwa hapo, au kutoka Bara na kuzoea mazingira, walikuwa hawashikiki kwa kupeana ujumbe mbalimbali uliokuwa unawasilishwa kwa nguo hizo.**

Kama nilivyosema, hivi sasa tabia hii haipo kabisa na kama ipo basi kwa kiasi kidogo sana, jirani wakigombana basi mmoja hutafuta kwa kununua kanga yenye ujumbe maalumu wa kumfumba jirani yake. Jioni mwenyewe huzivaa zile kanga na kukaa kibarazani nje na huhakikisha kwamba ule ujumbe jirani anausoma.

Jirani naye akitaka kujibu mapigo basi na yeye hutafuta kanga yenye msemo wa kujibu na yeye hufanya vile vile. Basi inakuwa malumbano tu kwa misemo ya khanga. Kanga na rusha roho ni pete na kidole. Hapo shughuli inakuwa ni kwa kinababa kugharamia ununuzi pasipo kujua nini kinafuata na wala hapewi nafasi.

Ujumbe utajulikana maana yake tu endapo utaweza kujua huyo mvaaji kamvalia nani. Jumbe nyingine ni za jumlajumla kwa watu wote lakini, zingine zinakuwa na mlengwa maalumu na kama ni mbea, au unajua sakata lolote baina yao basi ungejua mvaaji kamlenga nani.

Kwa mtindo wa kuvaa na kuvaliwa, kutoa ujumbe na kujibiwa ulisaidia wazalishaji na wafanyabishara kunufaika sana na biashara ya khanga kwa vijembe hivyo.

kuna mkasa mama mmoja alinisimulia kwamba hakumualika jirani yake kwenye sherehe, baada ya siku tatu akamuona amevaa khanga imeandikwa 'hata wewe nawe?" Akajua ujumbe ule ni wake, akaenda kumuomba msamaha, yakaisha.

Kulikuwa na ujumbe mbalimbali kwenye kanga kama: Umeyataka Mwenyewe; Wao Majungu Sisi Kazi tu; Chakubimbi Ukimuona Uogope; Mama Nipe Radhi Kuishi na Watu Kazi; Hasidi Hana Sababu; Sipandi Tena Mabasi Nimepata Yangu Basi; Yatakushinda.

Ujumbe mwingine kwenye kanga zilizokuwa zikivaliwa na kinamama ni Ukiwa Mroho Usiwe Mchoyo, Nilijua Mtabaki Labdalabda, Alaaah kumbeee, Chokochoko Mchokoe Pweza, Binadamu Hutamuweza, Heri Liwe, Roho Ziwatue, na Tupendanao Ndiyo Sisi Tupeni Nafasi.

**Sms: +255 716 350 534**





Rais Putin wa Urusi (kushoto) na Joe Biden wa Marekani

## Wanajeshi wanane wauawa nchini Mali

**BAMAKO,** MALI

JESHI la Mali limesema wanajeshi wanane wameuawa wakati wa shambulizi lililotokea eneo la magharibi mwa taifa hilo la ukanda wa Sahel, ambako wanamgambo wenye itikadi kali za dini ya Kiislam hufanya mashambulizi.

Idadi hiyo ya vifo ni mara mbili zaidi ya iliyotangazwa mapema.

Katika taarifa yao usiku wa kuamkia jana, jeshi hilo lilisema shambulizi hilo lililotokea Jumanne lilisababisha pia majeruhi kwa wanajeshi saba, magari mawili ya kijeshi yaliharibiwa na kwamba wanamgambo 31 waliuawa. Hatahivyo, taarifa hiyo haikutaja kundi lililohusika na shambulizi hilo

Nchi hiyo imekuwa kitovu cha mashambulizi ya wanamgambo yaliyoanzia kaskazini mwaka 2012, na kuenea hadi mataifa jirani ya Niger na Burkina Faso. Kufuatia machafuko hayo, maelfu ya watu katika ukanda huo wameuawa na takribani milioni mbili wameachwa bila makazi. **DW**

## Walinda amani washambuliwa

**BANGUI,** JAMHURI YA AFRIKA YA KATI

WANAJESHI watatu wa Tanzania wanaolinda amani katika Jamhuri ya Afrika ya Kati wamejeruhiwa jana wakati gari lao liliposhambuliwa kwa kilipuzi magharibi mwa nchi hiyo.

Taarifa hiyo ilitolewa na Ujumbe wa Umoja wa Mataifa MINUSCA, unaolinda amani katika Jamhuri ya Afrika ya Kati. Shambulizi hilo lilitokea juzi asubuhi wakati msafara wa walinda amani ulikuwa ukitoka mji wa Berberati, umbali wa maili 300 ukielekeamji mkuu Bangui. Afisa mmoja aliyejeruhiwa vibaya alisafirishwa hadi Bangui kwa matibabu. Umoja wa Mataifa umesema kwenye taarifa kuwa hii ni mara ya tatu walinda amani wa ujumbe wa MINUSCA wameshambuliwa kwa vilipuzi katika nchi hiyo.

Katika miezi ya hivi karibuni mgogoro wa muda mrefu kati ya waasi na vikosi vya serikali nchini humo umechukua mwelekeo tofauti. Waasi wametimiliwa kutoka miji mikuu lakini bado wanafanya mashambulizi ya kushtukiza na kutega mabomu ya ardhini. **DW**

# Marekani, Urusi sasa zaonyeshana ubabe

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Urusi Vladimir Putin amemuonya mwenzake wa Marekani Joe Biden kwamba kuiwekea vikwazo nchi yake kutokana na mgogoro wa Ukraine inaweza kusababisha kuvunjika kabisa kwa uhusiano.

Katika mazungumzo yao yaliyofanyika juzi kwa njia ya simu, Putin alisema vikwazo hivyo vitakuwa sawa na kosa kubwa.

Hata hivyo, Biden alimwambia Putin, kwamba Marekani na washirika wake watajibu kwa dhati uvamizi wowote utakaofanywa dhidi ya Ukraine.

Mazungumzo hayo ya simu yaliyoombwa na Urusi, ni ya pili kati ya viongozi hao wawili ndani ya mwezi uliopita na yalidumu kwa muda wa saa moja.

Ilikuwa ni juhudi za hivi punde za kutuliza mvutano kuhusu mpaka wa mashariki mwa Ukraine na Urusi, ambapo maofisa wa Ukraine wanasema zaidi ya wanajeshi 100,000 wa Urusi wamejikusanya.

Kuwepo kwa wanajeshi hao kumezua wasiwasi katika nchi za Magharibi, huku Marekani ikitishia vikwazo ambavyo hawajawahi kuviona.

Hata hivyo Urusi inakanusha kuwa inapanga kuivamia nchi hiyo na kusema kuwa wanajeshi wapo kwa ajili ya mazoezi. Ilisema ina haki ya kuhamisha wanajeshi wake kwa uhuru kwenye ardhi yake.

Ingawa pande hizo mbili zilipeana onyo wakati wa mazungumzo hayo, mshauri wa sera za kigeni wa Urusi Yuri Ushakov aliwaambia waandishi wa habari muda mfupi kwamba Rais Putin alifurahishwa na mkutano huo.

Ofisa Mkuu wa Marekani, ambaye alizungumza kwa sharti la kutotajwa jina, alisema sauti kwenye simu hiyo zilikuwa nzito.

Alisisitiza kwamba maendeleo makubwa katika mazungumzo hayo yanaweza kutokea tu katika mazingira ya kupunguzwa kwa mvutano na taharuki.

Katibu wa Vyombo vya Habari wa Ikulu ya White House Jen Psaki, alisema.

"Aliweka wazi kuwa Marekani na washirika wake watajibu vikali ikiwa Urusi itaivamia Ukraine".

Viongozi wa ngazi za juu wa Marekani na Urusi wanatazamiwa kukutana kwa mazungumzo ya ana kwa ana mjini Geneva mwezi huu.

Marais hao wawili wanaweza kufanyakazi pamoja kwa kuzingatia kuheshimiana na masilahi ya kitaifa ya kila mmoja. **BBC**

# Afrika Kusini kuondoa masharti dhidi ya corona

**CAPETOWN,** AFRIKA KUSINI

AFRIKA Kusini ambayo ni chimbuko la aina mpya ya kirusi cha corona, Omicron, imesema huenda wimbi la sasa la maambukizi limeshapita kilele chake na kwamba masharti yaliyowekwa kuyadhibiti maambukizi yanaweza kulegezwa.

Taarifa kutoka Ikulu ya Rais wa nchi hiyo imetoa tangazo hilo ambalo pia limeondoa marufuku iliyokuwepo ya kutembea nje usiku.

Kulingana na taarifa hiyo, maambukizi yalipungua kwa asilimia 30 wiki hii ikilinganishwa na wiki iliyopita.

Aidha, idadi ya wagonjwa wanaolazwa hospitalini pia ilipungua katika mikoa minane miongoni mwa tisa ya nchi hiyo. Maofisa hao walisema wimbi hilo halikusababisha ongezeko kubwa la vifo.

Kirusi cha Omicron ambacho kimetajwa kuambukiza kwa kasi kubwa baada ya kujibadilisha mara nyingi, kimesababisha ongezeko la maambukizi duniani wakati wa maandalizi ya kufunga mwaka. Hata hivyo ushahidi ukiwemo kutoka AfrikaKusini umeleta matumaini kwamba huenda kirusi hicho si hatari kama aina nyingine. **DW**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA INAUZWA

NYUMBA INAUZWA MOROGORO MJINI MASIKA MIL. 100. NI NZURI KWA BIASHARA, INA VYUMBA KUMI NA NNE. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU NAMBA**: **0745 222 312 / 0715 768 811.**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATRICE RENATUS MICHAEL** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUBARU FORESTER** yenye namba za usajili **T 643 DRV,** chasis namba **SH5020173** engine namba **EJ20EAA907289,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi tarifa **DAR/KIJ/RB/611208/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**ALICE GEORGE NCHWALI** anatangaza kupotelewa na kadi ya bajaji aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC 322 BGX,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **DAR/MBU/RB/611695/2021**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
Katika Mahakama ya mwanzo ya wilaya ya Njombe.
Kituo Cha Njombe Mjini
Mkoa wa Njombe
Usimamizi wa mirathi Na 59/2021

LUKA DAUDI NDENDYA------MAREHEMU
YUSTA AMOS MGAYA-------MSIMAMIZI

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANGAZO LA MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyotajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.

Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za miradhi hii yawe yameandikwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 24 ya mwezi Januari mwaka 2022.

**Imetolewa na hakimu Mkazi leo tarehe 24 desemba mwaka 2021.**

HAKIMU MKAZI
HAKIMU MKAZI
NJOMBE - MJINI

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**JAFET ODAS GABRIEL** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC. 413 BRS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya jeshi la polisi. **KAH/TR/RB/637/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya njombe**
**Kituo cha njombe mjini**
**Mkoa wa njombe**
**Shauri la madai/ndoa na 55 ya 2021**
**BARAKA MLAWA…………..mwombaji/mdai**
**HENRY MELEKION SALINGO……..mjibu maombi/mdaiwa**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**kanuni ya 15 (1) (2)ya kanuni za mashauri ya madai mahakama za mwanzo)**

**Kwa. HENRY MELEKION SALINGO WA ISITU**
**kwakuwa mdai ameleta madai yake kwamba UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI KUJIBU DAI LA KUKAZA HUKUMU**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 17 mwezi 01 mwaka 2022 saa 2:00 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyotee vinavyohusu shauri hii kwaajili ya kujitetea
**ANGALIZO**, kama hautoudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo
**Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 12 mwaka 2021**

Hakimu Mkazi

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI mkoa wa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi na 798/2021**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU……….HEMED ALLY OMARY NJECHELE**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA**
**NA ABDALAH OMARY NJECHELE**
**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowowte na mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 27 mwezi 1 mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo
Zingatia.endapo mtu yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa
**Imetolewa leo tarehe 24 mwezi 11 mwaka 2021**

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR-ES-SALAAM

***Uza, Chenye Thamani Kubwa***

***Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***

***Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-7

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

"Mjomba huyu ndiye yule kijana ambaye alinisaidia baada ya kukabwa na vibaka." Diana alimweleza mjomba wake.

"Karibu kijana, jisikie uko nyumbani." Mjomba alimkaribisha.

Diana alikuwa amemdanganya mjomba wake. Badala ya kumwambia alimkimbiza mwizi na kuuchukua mkoba ambao alikuwa ameporwa, yeye alimwambia kuwa alivamiwa na vibaka wanne, kijana huyo akajitokeza na kuwapiga wote na kukimbia.

Ilikuwa ni nia ya Diana kumfanya mjomba wake kukubali ujio wa Jan, vinginevyo aliona asingekubali.

Wakati chakula kikitengenezwa. Ni Diana aliyebaki na Jan na kuzungumza mengi.

Jan alimuelezea historia nzima ya maisha yake.

"Pole sana, ilitaka kufanana na ya kwangu tu."

Hakujua ni kitu gani kipo mwilini mwake. Diana alitokea kumpenda Jan. Lakini ilikuwa ni ngumu kumwambia.

Jan pia moyoni mwake alikuwa amekufa na kuoza kwa Diana. Tatizo alimuona ni maji marefu kwake.

Asingeweza kummudu kwani hali yake ya maisha anaijua mwenyewe. Chakula kililetwa na walikula kwa furaha. Kila mmoja alikuwa na furaha na lake moyoni.

Saa mbili ya usiku ilifika mapema kuliko ilivyotarajiwa. "Nasikitika kukwambia kuwa naondoka Diana." Jan alimtaka radhi. "Unaondoka?" aliuliza Diana kana kwamba hakutarajia kama Jan ataondoka siku hiyo.


"Ndiyo, unajua kuna kazi ya mtu fulani naenda kuifanya usiku huu huu, ili kesho nibakishe kazi moja tu kubwa."

"Siyo kama unamuwahi wifi yangu?" Lilikuwa ni swali la mtego.

Jan aliangua kicheko halafu akajibu "Sina. Sina yoyote yule mpaka sasa." alijibu akitabasamu na kusababisha Diana acheke.

"Mhh, hata mdomo wako unakusuta, unajibu huku unatabasamu."

"Ni kweli, basi we siku nishtukize tu useme nakuja nyumbani kwako, halafu kama utasikia nakwambia usije kwanza, labda kesho au kesho kutwa." alijibu jibu ambalo kwa mbali lilimrudishia amani Diana kuona Jan hakuwa na msichana yoyote.




**Jan na Diana walikuwa kwenye hoteli moja Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam, ambapo waliamua kukaa hapo kutwa nzima kwa ajili ya kufahamiana zaidi, Diana akilipia gharama zote.**

Diana alikuwa ametoka nje na mgeni wake, wadogo wake akiwa amewaacha ndani. Mjomba yeye baada ya kuona ugeni ule hakutaka kula naye. Aliwaachia uhuru vijana. Ni kwa sababu aliona wanahitaji maongezi marefu, wakiwa na uhuru bila wasiwasi wowote ule, hakutaka kuwabana. Alikula kivyake, halafu akaondoka.

Wakati Jan alipanda kwenye pikipiki lake, alichukua muda mrefu kumuangalia Diana kuanzia chini mpaka juu. Alionyesha kabisa kuwa kuna kitu moyoni mwake. Sasa Diana alikiona kitu hicho. Ni kama alisoma kwenye moyo wa Jan.

"Kwa heri Diana, tutaonana, nitakutumia meseji nikifika."

Diana alimuangalia Jan kwa jicho la kimahaba. Madaha ya kike, yalimuonyesha Jan kuwa amebakisha hatua chache tu kummiliki msichana huyo kama atakaza msuli.

"Nenda salama, ila kuwa muangalifu na magari, Mungu akutangulie."

"Amina."

Wakati Jan aliondoa pikipiki lake, Diana alibaki amesimama hapo hapo getini kwa muda mrefu. Kabla hajakata kona kuingia mtaa mwingine, aligeuza kichwa nyuma. Bado alimuona akiwa amesimama pale pale akimtazama. Kitendo cha kugeuza kichwa na kumtazama, kilimfanya Diana kunyoosha mkono wake juu na kumpungia kwa namna ya kumuaga. Na ndiyo wakati ambao Jan alikuwa amekata kona na kutokomea.

*********************************

Sasa alitambua kati ya wote watatu anampenda nani. Anayempenda ni Jan. Siyo mfanyabiashara Chala na wala si Afande Marco.

Pamoja na hayo hakutaka pia kuwapoteza hao wawili waliobaki. Akakumbuka jinsi Chala anavyomsaidia kwa pesa anazomtumia ambazo zinatatua shida mbalimbali.

Afande Marco naye kuna vitu ambavyo alikuwa akimsaidia. Ni vya kipolisi, kimahakama, hivyo naye pia hakutaka kumpoteza.

Tatizo ni kwamba aliyempenda zaidi hana kitu. Lakini hiyo haikumfanya amtenge.

Miezi mitatu ilipita. Kila mtu tayari alimuweka wazi mwenzake jinsi anavyompenda.

"Ni kweli nakupenda Jan, ila kuna kitu nataka kukwambia."

"Niambie tu."

"Ila utanisamehe sana mpenzi."

"Sawa, sema tu."

"Kabla ya kukutana na wewe, tayari nina uhusiano na wanaume wengine wawili."

Ni maneno yaliyomshtua Jan. Alijiona mwenye bahati mbaya. Wakati anakubaliwa tu, kuna vitu vinajitokeza.

Alijiuliza ni kwa nini Diana asingekataa? Kwa nini alionyesha tangu mwanzo kuwa anampenda bila masharti yoyote, bila pesa, lakini kumbe yuko kwenye uhusiano? Tena siyo wa mwanaume mmoja, wawili.

"Utanisamehe sana kwa sababu siyo kosa langu." Diana alisema, lakini Jan hakujibu kitu. Alionekana yupo mbali sana kimawazo.

"Jan?" Aliita Diana, baada ya kuona kama hayupo hapo.

"Naam." Alijibu kichovu.

"Usikasirike, mimi nimekwambia hivyo nina maana yangu. Sikutaka kukuficha chochote kile. Nilikuwa na uwezo wa kusema sina mtu yoyote na ningeweza kukuficha kwa kipindi ambacho mimi nahitaji nikufiche." Diana alimpoza Jan na yalikuwa ni maneno ambayo angalau yalionekana kumfariji na akili yake inaanza kurudi.

"Una maana gani kusema hivyo?"

"Ni hivi mpenzi. Siyo kosa langu ni Mungu amepanga hivi, sina uwezo wa kutengua. Ningeanza kukutana na wewe, hawa wawili nisingekuwa nao. Lakini nilikutana na mwanaume mmoja mfanyabiashara anaitwa Chala katika mazingira ambayo mimi sikuwa na mpenzi yoyote, achana na hawa wanaonifuatafuata. Halafu huyu mwingine ni askari, nilimpata nilipopata ajali ya bodaboda. Kwa bahati mbaya wewe nimekupata mwishoni. Na wewe ndiye nakupenda zaidi yao."

Jan na Diana walikuwa kwenye hoteli moja Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam, ambapo waliamua kukaa hapo kutwa nzima kwa ajili ya kufahamiana zaidi, Diana akilipia gharama zote. "Unasikia Jan, mimi nakuhitaji wewe na sitaki upate matatizo, kwa hiyo hili suala la hawa wawili niachie mimi, ila sitaki uwe na wivu kwa hivi sasa. Najua huko mbele ya safari nini nitafanya ili tubaki mimi na wewe. Nikisema eti leo nimekupata wewe, halafu niachane nao ghafla, kama nilivyokwambia mmoja ni mfanyabiashara mkubwa ana pesa balaa, anaweza kuweka wapelelezi na kujua ni kwa nini nimeamua kumuacha, akijua kuwa ni wewe, ndugu yangu umekwisha, anaweza kukuua kwa mbinu yoyote ile." Ni maneno ya Diana kuelekea kwa Jan, ambaye sasa aliamua kukaa kimya na kukubali matokeo.

Ni kweli hakuwa na uwezo kipesa, wala cheo kuliko hao. Pia ndiyo walioanza nao. Yeye ajione tu mwenye bahati ya kukubaliwa na msichana mrembo.

ITAENDELEA JUMAMOSI

HABARI MICHEZO

# WACHEZAJI WALALAMA JOTO SARE NAMUNGO, BIASHARA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kumalizika kwa sare ya bao 1-1, mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya wenyeji Namungo FC dhidi ya Biashara United kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi hapo juzi, wachezaji wa timu zote mbili wamelalamika hali ya joto lililotokana na jua kali, imeelezwa.

**Wachezaji wa timu hizo walisema hali hiyo iliwafanya washindwe kuonyesha ubora wao katika mchezo huo wa raundi ya 11.**

"Tulikuwa nyumbani ndiyo, lakini tulicheza kwenye mazingira magumu, jua lilikuwa kali sana kwa hiyo wachezaji tulicheza kwa nguvu, lakini baadaye tulichoka kwa sababu hali ya hewa haikuwa nzuri, lakini tunashukuru hata kwa hiki kidogo tulichopata," alisema Reliant Lusajo, nyota wa Namungo FC.

Naye winga wa Biashara United, Dennis Nkane, alisema ilikuwa mechi ngumu kutokana na hali ya hewa kutokuwa rafiki kwa wachezaji.

Nkane alisema wachezaji wa timu zote mbili walikutana na wakati mgumu lakini wanashukuru Mungu mchezo huo ulimalizika salama na hakuna mchezaji ambaye aliathirika zaidi kiafya.

"Hatukuzoea kucheza na hali ile, jua lilikuwa kali sana, ndiyo maana kuna wakati tulicheza kwa tahadhari na watu wakaona kama vile tunazuia sana, lakini ilibidi tupumzike ili tusichoke sana kutokana na joto," alisema Nkane ambaye inasemekana juzi ilikuwa ni mechi yake ya mwisho, kabla ya kutangazwa kujiunga na klabu ya Yanga ya jijini Dar es Salaam.

Wachezaji waliofunga mabao katika mechi hiyo walikuwa ni Lusajo dakika ya tisa kwa upande wa wenyeji kabla ya Nkane kusawazisha dakika ya 38.

Ni Matokeo ambayo yameipeleka Namungo katika nafasi ya nane kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa imecheza mechi 11 na kujikusanyia pointi 13 wakati Biashara United ikipanda nafasi moja, kutoka kuburuza mkia hadi kwenye nafasi ya 15 na pointi zao tisa mkononi.

Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara mzunguko wa 11 unatarajiwa kukamilika leo kwa Simba kuvaana na Azam FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa na baada ya hapo ligi hiyo itasimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kufanyika Zanzibar kuanzia kesho.



Winga wa Namungo FC, Shiza Kichuya (kushoto), akijiandaa kumtoka beki wa Biashara United, Abdallah Madirisha katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Ilulu, Lindi juzi. Timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mzambia atua kuinoa Namungo FC

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Kocha wa Timu ya Taifa ya Zambia, Honour Janza, ametangazwa rasmi kuchukua mikoba ya iliyoachwa na Hemed Morocco, kuinoa Namungo FC inayoshiriki Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, imefahamika.

Janza alikuwa jukwaani juzi kushuhudia mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara kati ya Namungo dhidi ya Biashara United ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.

Katibu Mkuu wa Namungo, Ally Selemani aliliambia gazeti hili mazungumzo na kocha huyo yamefikia hatua nzuri na tayari ameshasaini mkataba wa ajira yake hiyo mpya.

Selemani alisema wamefikia hatua hiyo baada ya kukamilika kwa taratibu zote na sasa wanaamini kocha huyo mpya atairejesha Namungo kwenye ushindani.

"Honour Janza ndio kocha wetu mkuu, muda wowote kuanzia leo (jana), tutamtambulisha ili aanze kazi rasmi katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi," alisema katibu huyo.

Aliongeza uongozi wa timu hiyo una matarajio makubwa na kocha huyo na wanaamini chini yake watafikia malengo ya kumaliza katika nafasi tano za juu kwenye Ligi Kuu.

Janza amerithi mikoba ya Morocco aliyejiuzulu mapema wiki hii baada ya kuona timu hiyo ina mwenendo mbaya wa timu hiyo.

# Zimamoto yasaka mastraika watatu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

ILI kuimarisha kikosi chake kinachoshiriki Ligi Kuu Zanzibar, Kocha Mkuu wa Zimamoto, Mohammed Hilalry "Kocha Tedy" amesema anahitaji kusajili washambuliaji watatu wapya.

Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), limetangaza dirisha dogo la usajili litafunguliwa rasmi kuanzia keshokutwa hadi Januari 20, mwaka huu.

Kocha Tedy alisema baada ya kubaini kikosi chake kinamapungufu katika idara ya ushambuliaji, amelazimika kusajili washambuliaji wengine ili kuiongezea nguvu timu yake.

Kocha huyo alisema changamoto hiyo imesababisha timu yake kushindwa kuonyesha makali katika mechi za mzunguko wa kwanza ambazo zimemalizika.

Aliongeza tayari ameshawasilisha mapendekezo yake kwa uongozi wa timu hiyo na anaamini endapo watatekeleza, watarejea kwenye mzunguko wa lala salama wakiwa imara.

"Tulianza vizuri katika michezo ya mwanzo pale msimu ulipoanza, lakini baadaye tulipoteza mechi, hii inatokana na changamoto ya kutokuwa makini kwa washambuliaji, lakini pia hata waamuzi baadhi walishindwa kutafsri vyema sheria au walifanya makusudi," alisema kocha huyo.

Alisema katika usajili mpya anaotarajia kuufanya, hana mpango wa kuchukua wachezaji kutoka nje ya Zanzibar na 'macho' yake ameyaelekeza kwa nyota wa timu nyingine zinazoshiriki ligi hiyo ya juu visiwani humo.

"Ni mapema kuweka wazi majina ya wachezaji nitakaowasajili, ila watatoka katika vilabu vya Ligi Kuu Zanzibar, nikifanikiwa kuwapata, mambo kwetu yatakuwa mazuri," Kocha Tedy alisema.

Aliongeza ligi hiyo imezidi kuwa na ushindani na ngumu kutokana na kila timu inayoshiriki kufanya usajili wenye malengo na udhamini uliopatikana.

"Ni ngumu mpaka sasa kutabiri timu ipi itakuwa bingwa kwa sababu timu zote zinapambana kuhakikisha zinaukwaa ubingwa wa Zanzibar msimu huu," aliongeza.

Zimamoto ipo nafasi ya tisa katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar ikiwa na alama 23 baada ya kucheza michezo 15.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SAKA ATAKIWA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool inavutiwa na winga wa Arsenal na England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20, ambaye mkataba wake kule Emirates utamalizika ifikapo mwaka 2024. ***(Transfer Window podcast, via Express)***

### LIVERPOOL YAMTAKA KESSIE

LIVERPOOL pia wametoa ofa ya mkataba kwa kiungo wa kati wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake San Siro unakamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Ansa)***

### LAPORTE ANUKIA BARCA

KLABU ya Barcelona inataka kumsajili beki wa Manchester City na Timu ya Taifa ya Hispania, Aymeric Laporte mwenye umri wa miaka 27 msimu ujao. ***(Sun)***

### BOTMAN KUTUA NEWCASTLE

NEWCASTLE inakaribia kumnunua mlinzi wa Lille Mholanzi aliyekadiriwa kuwa na thamani ya pauni milioni 30, Sven Botman (21), kama sehemu muhimu ya biashara yao ya uhamisho wa Januari. ***(Mail)***

### RAMSEY AGOMBEWA EPL

NEWCASTLE pia wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Juventus kutoka Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 31, huku West Ham na Everton pia wakimtaka mchezaji huyo. ***(Sun)***

### DEMBELE AKARIBIA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle imeweka ofa ya mkataba "mkubwa" kwa winga wa Barcelona ambaye hana utulivu, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24. ***(Rudy Galetti on Twitter)***

### ARSENAL YAMTAKA ISAK

ARSENAL imewatambua nyota wa Real Sociedad na Uswisi, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 22, na nyota wa Lille na Canada, Jonathan David (21), kama chaguo linalowezekana ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(The Athletic)***

### CHELSEA YAINGIA SOKONI

CHELSEA wanakaribia kumnunua kiungo wa kati wa Monaco Mfaransa Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21, ambaye anaweza kuwa chaguo nafuu kuliko nyota wa West Ham na England, Declan Rice (22). ***(Daily Telegraph)***

### LYON YAIGOMEA CHELSEA

LYON imekataa jaribio la Chelsea la kutaka kumnasa beki wa kushoto wa Italia, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 27, ambaye yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Ligue 1. ***(L'Equipe, via Get French Football News)***

### SIMEONE ATAJWA LEEDS

LEEDS United wanataka kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Giovanni Simeone mwenye umri wa miaka 26, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Verona akitokea Cagliari, majira ya joto. ***(L'Arena, via Sport Witness)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# DEMBELE, BARCA MAMBO MAGUMU

**Mazungumzo ya kusaini mkataba mpya yavunjika baada ya Mfaransa huyo...**

**BARCELONA,** Hispania

MKUTANO kati ya wawakilishi wa winga Ousmane Dembele na Barcelona umevunjika baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa ESPN.

Na sasa Dembele huenda akaondoka Barcelona msimu unaokuja wa majira ya joto baada ya mazungumzo ya kuongeza mkataba na klabu hiyo kuvunjika.

**Mazungumzo hayakwenda kama vile Barcelona walivyotarajia na maombi ya mkataba wa Dembele hayakutimizwa.**

Na kubwa zaidi lililosababisha kuvunjika kwa mazungum zo hayo ni kuhusu mapendekezo ya mshahara unaotakiwa na Dembele.

Hata hivyo, kocha Xavi na uongozi wamebakia na matumaini makubaliano yanaweza kuafikiwa licha ya hali mbaya iliyojitokeza.

Mkataba wa sasa wa Dembele unamalizika msimu huu na yuko huru kufanya mazungumzo ya awali ya mkataba na klabu nyingine kuanzia leo Januari Mosi.

Matumaini yalikuwa kwa Barcelona kufikia makubaliano na winga huyo wa Ufaransa kabla ya tarehe hiyo, lakini mazungumzo ya wiki hii yalivurugika pale Dembele alipokataa kukatwa mshahara.


CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 804

MECHI KALI
HOME AWAY
SIMBA
1.62 | 3.46 | 5.19
AZAM

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ICARDI ATAJWA KUMRITHI CAVANI



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kumtambua, Mauro Icardi wa Paris Saint-Germain kama mbadala wa Edinson Cavani kwenye dirisha dogo la usajili la Januari.

Cavani anaaminika yuko njiani kuondoka katika kikosi cha Mashetani Wekundu hao mwanzoni mwa 2022, huku Barcelona wakiibuka kuongoza mbio za kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay, ambaye mkataba wake unamalizika Old Trafford ifikapo Juni.

Kwa mujibu wa Calciomercato, Manchester United tayari wanajiandaa kwa ajili ya uhamisho wa mshambuliaji huyo na wanamwona Icardi kama mchezaji anayefaa kuchukua nafasi ya Cavani.

Hata hivyo, United wanatajwa na vyanzo kadhaa huenda wasifanye manunuzi yoyote kwenye soko la Januari wakijaribu kupunguza ukubwa wa kikosi chao.

Lakini ripoti ya Calciomercato inadai kuwa Juventus pia wanatamani sana kumnunua Icardi katika usajili wa Januari.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, ambaye pia anahusishwa na Chelsea na Arsenal, ametikisa nyavu mara tano katika mechi 20 akiwa na PSG wakati wa msimu wa 2021-22.

## Tuchel: Chelsea ngumu kutwaa taji



**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Ruchel amekiri kuwa kutokana na changamoto kadhaa, ni ujinga kudhani kuwa kikosi chake kinaweza kutwaa taji msimu huu.


Chelsea waliruhusu bao la kusawazisha dhidi ya Brighton dakika ya 91 Jumatano, huku Reece James na Andreas Christensen wakiungana na orodha ndefu ya majeruhi kwa klabu hiyo.

Kwa sasa, Chelsea wapo nyuma ya vinara wa Ligi Kuu England, Manchester City kwa pointi nane, na matumaini ya mbio za ubingwa yanayoyoma kwa sababu ya changamoto za Covid-19 na orodha kubwa ya majeraha ya wachezaji muhimu walionao.

Akizungumzia juu ya matumaini ya Chelsea kwenye mbio za ubingwa, Tuchel amesema kuwa ni ujinga kufikiria klabu hiyo inaweza kutwaa ubingwa kwa mwaka huu.

"Tunaweza kuwajinga kufikiri tunaweza kwa changamoto ya Covid na majeruhi," alisema Tuchel akinukuliwa na BBC Sport.

HABARI MICHEZO



4,667,160

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.02/01/21 | 17:00 | Brentford vs Aston Villa | 2.96 | 3.26 | 2.41 |
| 02.02/01/21 | 17:00 | Everton vs Brighton | 2.70 | 3.20 | 2.65 |
| 03.02/01/21 | 17:00 | Birmingham vs QPR | 2.57 | 3.11 | 2.71 |
| 04.02/01/21 | 18:00 | Montpellier vs Strasbourg | 2.47 | 3.25 | 2.76 |
| 05.02/01/21 | 18:00 | Queen of South vs Hamilton | 2.49 | 3.28 | 2.64 |
| 06.02/01/21 | 18:00 | Arbroath vs Inverness | 2.44 | 3.09 | 2.84 |
| 07.02/01/21 | 18:00 | Alloa Athletic vs Falkirk FC | 2.74 | 3.22 | 2.44 |
| 08.02/01/21 | 18:00 | Stenhousemuir vs Stirling | 2.34 | 3.38 | 2.66 |
| 09.02/01/21 | 18:15 | Elche vs Granada | 2.47 | 3.10 | 3.00 |
| 10.02/01/21 | 19:30 | Chelsea vs Liverpool | 2.95 | 3.45 | 2.32 |
| 11.02/01/21 | 20:30 | Alaves vs Real Sociedad | 3.36 | 3.11 | 2.27 |
| 12.02/01/21 | 23:00 | Mallorca vs Barcelona | 3.30 | 3.21 | 2.24 |
| 13.02/01/21 | 23:00 | Fuenlabrada vs UD Ibiza Eivissa | 2.27 | 2.95 | 3.34 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 01 - JANUARI 2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 2958 | Shahrdari Astara vs Vista Turbine | 2.21 | 2.70 | 3.62 |
| 13:30 | 1077 | Shams Azar Qazvin vs Esteghlal Mollasani | 1.84 | 2.80 | 5.03 |
| 13:30 | 1304 | Saipa Karadj vs Malavan Bandar Anzali | 3.14 | 2.56 | 2.56 |
| 13:30 | 1832 | Esteghlal Khuzestan vs Shahrdari Hamedan | 1.93 | 2.89 | 4.24 |
| 13:30 | 2359 | Kheybar Khorramabad FC vs Machine Sazi Tabriz | 1.14 | 5.96 | 17.30 |
| 13:30 | 3924 | Mes Shahr-e Babak vs Ghasghaei Shiraz | 2.31 | 2.70 | 3.37 |
| 13:30 | 4684 | Pars Jonoubi Jam vs Arman Gohar Sirjan | 3.42 | 2.60 | 2.37 |
| 15:25 | 5454 | Al Taawon vs Dhamk | 2.09 | 3.56 | 3.22 |
| 15:30 | 2708 | Sheffield Utd vs Middlesbrough | 2.09 | 3.28 | 3.38 |
| 15:30 | 4508 | Thailand vs Indonesia | 1.38 | 4.43 | 6.74 |
| 15:30 | 5832 | Arsenal vs Manchester City | 5.12 | 4.26 | 1.59 |
| 15:45 | 1756 | Abha vs Al Raed Club | 2.51 | 3.45 | 2.61 |
| 15:50 | 3282 | AL Tawon SC vs Hatta Club | 4.99 | 4.23 | 1.51 |
| 15:50 | 4220 | Dibba Al Fujairah vs Dubba Al-Husun | 1.59 | 4.04 | 4.52 |
| 15:55 | 5204 | Al-Hamriyah vs AL Arabi | 2.60 | 3.51 | 2.32 |
| 16:00 | 2730 | Thagafi Tulkarem vs Markez Tulkarm | 1.52 | 4.14 | 5.00 |
| 16:00 | 5066 | Hapoel Tel Aviv vs Maccabi Petach Tikva | 2.14 | 3.23 | 3.09 |
| 17:40 | 4731 | Al Fateh (KSA) vs Al Nasr Riyadh | 6.93 | 5.15 | 1.37 |
| 18:00 | 1253 | Oxford Utd vs Cheltenham | 1.59 | 3.91 | 5.08 |
| 18:00 | 1341 | Glenavon vs Cliftonville Belfast | 2.74 | 3.32 | 2.30 |
| 18:00 | 1834 | Blackpool vs Hull City | 2.06 | 3.39 | 3.34 |
| 18:00 | 2014 | Radcliffe Borough vs Utd of Manchester | 2.70 | 3.33 | 2.33 |
| 18:00 | 2125 | Hartlepool vs Oldham | 2.05 | 3.33 | 3.43 |
| 18:00 | 2252 | Forest Green vs Stevenage | 1.55 | 3.93 | 5.50 |
| 18:00 | 2823 | MK Dons vs Gillingham | 1.52 | 4.15 | 5.53 |
| 18:00 | 3371 | Burton vs Crewe | 1.77 | 3.59 | 4.23 |
| 18:00 | 3473 | Watford vs Tottenham | 5.02 | 4.12 | 1.62 |
| 18:00 | 3505 | Swindon Town vs Northampton | 2.08 | 3.39 | 3.29 |
| 18:00 | 3534 | Scunthorpe vs Carlisle | 2.80 | 3.20 | 2.44 |
| 18:00 | 3672 | Ballymena Utd vs Portadown FC | 1.59 | 3.85 | 4.72 |
| 18:00 | 3675 | Hendon vs Kings Langley | 1.82 | 3.86 | 3.42 |
| 18:00 | 3781 | Barrow vs Bradford City | 2.42 | 3.18 | 2.83 |
| 18:00 | 4085 | Charlton vs Wycombe | 2.25 | 3.30 | 3.00 |
| 18:00 | 4309 | Walsall vs Newport | 2.52 | 3.26 | 2.66 |
| 18:00 | 4619 | Coleraine FC vs Warrenpoint | 1.19 | 5.97 | 10.59 |
| 18:00 | 4803 | Leatherhead vs Kingstonian | 4.25 | 3.62 | 1.70 |
| 18:00 | 4918 | Jabal EL Mokaber vs Shabab Al Dhahiriya | 1.65 | 3.63 | 4.55 |
| 18:00 | 4934 | Crusaders Belfast vs Carrick Rangers | 1.34 | 4.72 | 7.12 |
| 18:00 | 4956 | Tamworth vs Hednesford Town | 2.27 | 3.70 | 2.90 |
| 18:00 | 5091 | Dungannon Swifts vs Linfield Belfast | 14.46 | 7.33 | 1.12 |
| 18:00 | 5546 | Rotherham vs Bolton | 1.44 | 4.53 | 6.11 |
| 18:00 | 5579 | Leyton Orient vs Bristol Rovers | 1.95 | 3.44 | 3.63 |
| 18:30 | 5321 | Ironi Kiryat Shmona vs Hapoel Haifa | 2.94 | 3.19 | 2.24 |
| 19:00 | 2765 | Simba vs Azam | 1.62 | 3.46 | 5.19 |
| 19:00 | 4319 | Hapoel Katamon vs Hapoel Hadera | 2.94 | 2.99 | 2.35 |
| 19:50 | 2859 | Al Ahli Jeddah vs Al Shabab Riyadh | 3.22 | 3.57 | 2.08 |
| 20:30 | 4647 | Glentoran Belfast vs Larne | 2.13 | 3.52 | 2.89 |
| 20:30 | 5536 | Crystal Palace vs West Ham | 3.01 | 3.46 | 2.28 |
| 20:50 | 1357 | Maccabi Netanya vs Beitar Jerusalem | 2.26 | 3.09 | 2.99 |
| 22:30 | 2395 | WAF Widad Fes vs Club Jeunesse Ben Guerir | 2.03 | 2.81 | 3.97 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# KAZE AFUNGUKA YACOUBA BADO ANA NAMBA YANGA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema mshambuliaji, Yacouba Songne bado ataendelea kuitumikia klabu hiyo kwa sababu bado ana nafasi katika kikosi cha timu hiyo licha ya kusajili wachezaji wengine wapya wa kimataifa.

Kaze ametoa kauli hiyo ni baada ya kuwapo kwa tetesi Songne jina la nyota huyo linaweza kuondolewa ndani ya kikosi cha Yanga kutokana kukaa nje ya dimba kwa muda mrefu.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Kaze alisema kwa sasa hawana mpango wa kumwondoa moja kwa moja nyota huyo kikosini kwa sababu wanafahamu bado anauguza majeraha lakini wanathamini kiwango chake.

Alisema mchezaji huyo ataendelea kubaki ndani ya kikosi cha Yanga huku akifanya mazoezi mepesi chini ya uangalizi wa madaktari mpaka pale hali yake itakapoimarika.

"Tukiwa tunaendelea kutafuta mshambuliaji mwingine kwa ajili ya kuimarisha safu ya ushambuliaji, lakini uamuzi wa kutafuta mshambuliaji mwingine hautaleta maana Yacouba anaondolewa kwenye mipango yetu moja kwa moja," alisema Kaze.

Alisema wanaamini mara mshambuliaji huyo atakapopona, atarejea kwenye kikosi na kuisaidia timu hiyo ifikie malengo yake.

Aliongeza kikosi chao kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar ambayo yanatarajiwa kutimua vumbi kuanzia kesho huko Unguja.



Wachezaji wa Azam FC wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya Simba itakayochezwa leo usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

# *Pisha nikupishe usajili Ligi Kuu Bara*

**Na Adam Fungamwango**

USAJILI wa Ligi Kuu Tanzania Bara umezidi kupambana moto, timu zikichukuliana wachezaji huku akitoka huyu na mwingine kule kwa ajili ya kuimarisha vikosi vyao katika dirisha dogo la usajili ambalo lilifunguliwa tangu Desemba 15, mwaka jana.

Wakati kipa aliyesajiliwa mwanzoni mwa msimu huu wa Simba, akiondoka na kwenda Mtibwa Sugar, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Ibrahim Ajibu naye ameondoka kwenye kikosi hicho na kujiunga na Azam FC.

Tayari klabu ya Yanga, Jumatano iliyopita ilimtambulisha golikipa, Aboutwalib Mshery kutoka Mtibwa Sugar muda mfupi tu baada ya kutoka kucheza mechi ya Ligi Kuu, kati ya wakata miwa hao dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani Tanga.

Ilikuwa ni baada ya kumtambulisha, Salum Abobakar kutoka Azam FC, huku ikitarajia kumtambulisha winga, Dennis Nkane kutoka Biashara United, wakati wowote kuanzia jana. Dodoma Jiji nayo Jumatatu ilimtambulisha straika wa zamani wa Yanga, Waziri Junior.

Geita Gold ambayo imeonekana kutia fora kwenye kipindi hiki cha usajili, imemsajili kipa, Aron Kalambo kutoka Prisons, Adeyum Salim kutoka Yanga, huku tayari ikiwa na Ditram Nchimbi kutoka Yanga, Juma Nyosso, na kiungo wa zamani wa Simba William Lucian 'Gallas'.

Simba nayo inadaiwa iko kwenye harakati za kutaka kumsajili beki wa pembeni wa Coastal Union, Hans Masoud.

Mtibwa Sugar nayo ilimtambulisha winga wa zamani wa Simba na TP Mazembe, Deo Kanda ingawa inadaiwa pia ameshasajili na timu ya Ligi ya Championship, Kitayosce ya Tabora.

Michezo

Jumamosi Januari 1, 2022

Nipashe



Dembele, Barca mambo magumu UKURASA 21



Straika wa Simba, Chriss Mugalu (kushoto), akiwania mpira dhidi ya beki wa timu hiyo, Paschal Wawa kwenye mazoezi ya kujiandaa kuikabili Azam FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo usiku. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba, Azam mtifuano

## ●●● Ni mechi nyingine ya 'kibabe' ya Ligi Kuu inayotarajiwa...

**Na Saada Akida**

MECHI kali na ya ufundi inatarajiwa kuonekana leo wakati mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara , Simba watakapovaana na Azam FC kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Simba huenda itaingia katika mchezo huo ikiwa bado inakosa huduma ya straika wake, Chris Mugalu ambaye alikuwa majeruhi wa muda mrefu lakini Azam FC itawakosa wachezaji watatu ambao ni Bruce Kangwa, Never Tigere na Prince Dube ambao wako katika majukumu ya Timu ya Taifa ya Zimbabwe, iliyoko Cameroon kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022).**

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema wamejiandaa vizuri na wataingia katika mchezo huo kwa kazi moja ya kutafuta pointi tatu muhimu. Pablo alisema mchezo huo ni muhimu sana kwao kwa sababu mbali na kuhitaji ushindi, pia wanataka kufungua mwaka mpya wa 2022 kwa furaha.

Alisema wachezaji wake wote wako fiti na tayari kwa ajili kupambana ili kuvuna pointi zitakazowaimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini.

Mhispania huyo alisema ana imani mchezo huo utakuwa wa kiufundi na mbinu zaidi kutokana na aina ya wachezaji walioko kwenye vikosi viwili vya timu hizo.

"Azam FC iko vizuri, ina wachezaji wazuri lakini hata Simba tumejipanga vizuri kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri, tumefanyia kazi ubora na madhaifu ya wapinzani wetu kwa lengo la kuondoka na matokeo chanya," alisema Pablo.

Kuhusu kuondoka kwa Ibrahim Ajibu, Pablo alisema ni mchezaji mzuri na mwenye kipaji lakini ameshindwa kupata namba kwenye kikosi cha Simba kutokana na ubora wa wachezaji waliopo ndani ya mabingwa hao watetezi.

"Ajibu ni mchezaji mzuri lakini kwa Simba hakupata nafasi, namtakia kila la kheri alipokwenda lakini haitaathiri wachezaji wangu kuelekea mchezo wetu dhidi ya Azam FC, malengo yetu ya kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wa kesho (leo), yapo pale pale," alisema Pablo.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Iddy Abubakar alisema wamejiandaa vizuri na wanafahamu Simba ni timu kubwa, hivyo wataingia katika mechi hiyo kwa tahadhari kubwa ili kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

Iddy alisema kukosekana kwa wachezaji wao watatu haitaathiri mipango yao ya 'kuimaliza' Simba kwa sababu wamejiandaa vyema kuvuna pointi tatu katika mchezo huo ambao ni muhimu kwao.

"Tutacheza kwa tahadhari kubwa, tunajua Simba ni timu bora na imara, na pia kila mechi wanabadilika, wakati tukiingia na mbinu zetu lakini huku tutatumia dakika 15 za mwanzo kuwasoma Simba na kuhakikisha tunafikia malengo yetu ya kutafuta pointi tatu muhimu," alisema Iddy.

Baada ya mechi hii ya mwisho ya raundi ya 11, Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itasimama kwa muda kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia kesho huko Zanzibar.

Ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itarejea tena kuanzia Januari 14, mwaka huu.

Timu za Tanzania Bara zilizoalikwa katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi ambayo hufanyika kila mwaka ni pamoja na Simba, Yanga, Azam FC zote za jijini na Namungo kutoka mkoani Lindi.

# Yanga kuhamishia makali Mapinduzi

**Na Saada Akida**

VINARA wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Yanga, wametamba wako imara na kamili kuendelea kutoa 'dozi' kwa kila timu watakayokutana nayo kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi huko Zanzibar.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia gazeti hili wanakwenda Zanzibar na wachezaji wao wote isipokuwa ambao ni majeruhi kwa sababu wanataka kurejea na ubingwa wa michuano hiyo.

Kaze alisema kila mchezaji wa Yanga anafahamu malengo waliyokuwa nayo msimu huu, hivyo wameahidi kuhamishia 'makali' yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye mashindano hayo.

"Tunataka kuendelea kufanya vizuri katika kila mashindano tunayoshiriki, kikosi chetu kimeimarika na kiko tayari kwa ajili ya kupata ushindi," alisema Kaze.

Aliongeza kila mechi kwao sasa ni sawa na fainali kwa sababu wanataka kukaa kileleni na si kwenye nafasi za chini.

"Tumejiandaa kukutana na ushindani, tunajua tutakutana na timu zilizojipanga pia, mechi zetu zote ni sawa na fainali, tunaingia kwa ajili ya kusaka ushindi tu," alisema Kaze.

Katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Yanga imepangwa Kundi B ikiwa pamoja na Taifa Jang'ombe na KMKM wakati Simba iko Kundi C na Selem View na Mlandege wakati Kundi A linaundwa na Azam FC, Namungo, Yosso Boys na Meli 4 City.

Yanga ambayo ilitolewa mapema katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, pia inashiriki michuano ya Kombe la FA.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >